SportPesa

CHEZA USHINDE SASA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa


**SHUKRANI**

**UONGOZI na wafanyakazi wa gazeti hili unapenda kuwashukuru wasomaji na watangazaji wote kwa ushirikiano mkubwa katika kipindi chote cha mwaka 2021. Wakati tukiukaribisha mwaka 2022 tunawatakia kila la heri katika shughuli zenu kwa kutimiza malengo mliojiwekea. Tunaomba ushirikiano huu uendelee kudumu.**

**Mhariri**


Hebu tukae chini na tutafakari majina haya!

Ukurasa 13

BUFE

IJUMAA DESEMBA 31, 2021 Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

MUHOGO SASA UNALIPA...
TOSCI yawavusha wakulima, wadau wake kutoka 'mbegu zembe' hadi mpya kisasa

Ukurasa 12

**Mwekezaji mzawa Lake Oil ajitosa kuhudumia mafuta viwanja ndege**

- Dhamira ya 2018 inaanzia KIA, Iringa, Dar
- Meneja: Tumeajiri 6000, akiba ipo lita mil 18

**Na Julieth Mkireri**

RAI na kilio kikubwa katika uongozi kitaifa, kwa awamu mbalimbali inayojumuisha ya sasa, dhima ni kuongeza uwekezaji kwa kiasi kikubwa, safari kuelekea Tanzania ya Viwanda, ambayo nchi sasa imeshakanyanga.

Ni tafsiri ambayo ndani yake kuna dhana ya uwekezaji kiuchumi, ambayo inafungua mengi katika safari ya maendeleo kitaifa, kuongeza pato la kodi kitaifa, ajira kwa umma, na mzunguko wa fedha wenye sura ya kukuza uchumi.

Hapo kuna suala la kuongezeka pato la mtu mmoja mmoja, vitengo vinabadilishana maisha hadi kufikia ngazi ya kaya.

Ndani ya suala la kuhamasisha uwekezaji wa ndani ya nchi, wenye tafsiri inayojumuisha kuweka msukumo wa maendeleo katika sura ya kimataifa, pia wakati.

Uhamasishaji wa kaulimbiu ya Tanzania ya Viwanda, umeenda sambamba na kuboresha mazingira ya uwekezaji, ikiwamo kuondoa vikwazo vilivyokuwa vikielezwa awali katika taasisi wezeshi.

Kuna sekta ya gesi na mafuta ambako bidhaa petroli inatumika kwa wingi nchini, kwa matumizi ya nyenzo za usafiri kitaifa na kimataifa, ndege, treni, magari. Vivyo hivyo ni katika matumizi ya nyenzo kama jenereta.

Mafuta ni nyenzo muhimu, ambayo biashara yake inaendeshwa na kampuni nyingi, kuanzia zinazomiliki huduma za usafiri kama treni, lakini wengi ni wamiliki binafsi wanaowauzia wahitaji .

Hapo ndiko inakopatikana kampuni ya Lake Oil, yenye zaidi ya miaka 10 iliyopita, ikijishughulisha na usambazaji mafuta, ndani na nje ya Tanzania, ikijenga vituo vyake vya mafuta ndani ya Afrika Mashariki.

Meneja Mshauri wa Kitengo cha Anga, Ismail Elagib, anaiambia Nipashe kuwa, mbali na uamuzi wa kusogeza huduma karibu waliko wateja, mjini na vijijini, pia imeanza kutoa huduma ya mafuta ya ndege kwenye usafiri wa anga

Ismail anafafanua kwamba, kampuni hiyo imeshapatiwa kibali cha kuanza kutoa huduma katika viwanja vitatu vya ndege nchini, ambavyo ni Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA), Kiwanja cha Ndege cha Iringa na Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Meneja huyo anaeleza kwamba katika mikakati ya kuongeza uwekezaji nchini, walipata wazo la kuanza kuhudumia kwenye usafiri wa anga tangu mwaka 2018 na mwezi uliopita - Novemba, ndio walianza kutoa huduma hiyo baada ya kukamilisha uwekezaji KIA, akifafanua kwa sasa wamekamilisha ujenzi wa miundombinu katika kiwanja hicho cha ndege.

Meneja Mshauri wa Kitengo cha Anga wa Lake Oil, Ismail Elagib. PICHA: JULIETH MKIRERI.

Pia, anafafanua kwamba Novemba 25, mwezi mmoja uliopita walishaanza kutoa huduma katika viwanja vya Iringa. Anasema katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, wanatarajia kuanza kuhudumia mwaka ujao 2022, unaoanza kesho, baada ya kukamilisha taratibu stahiki.

Anataja malengo yao katika miaka mitano ijayo wanakoelekea, ni kufikisha huduma bora katika viwanja vinginevyo, akifafanua wana maono yao, kufika Tanzania Visiwani na nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Ismail anaeleza kwamba, uwekezaji huo katika kusambaza mafuta ya ndege kwenye huduma za anga, unazingatia mwongozo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Shirikisho la Mamlaka za Anga Duniani (IATA) na Muunganiko wa Kimataifa wa Usimamizi wa Mambo ya Mafuta ya Ndege (JIG).

Ismail anaeleza kwa sasa, kampuni hiyo ina jumla ya wafanyakazi 6,000 na kati yao wa kitengo cha anga wapo 16, wakijumuisha wabobezi kwenye tasnia ya mitambo na oparesheni ya mafuta ya ndege nchini, wanaotegemea kuongezeka baadae, kulingana na huduma zitakavyokuwa zikiongezeka.

"Lengo letu ni kutoa huduma bora na nafuu. Mipango mikakati yetu ni kufikia viwanja vya ndege katika mikoa yote hapa nchini na baadae nchi jirani," anaeleza.

Meneja huyo anafafanua kwamba, hadi sasa wataendelea kujifunza kwa kampuni nyinginezo zinazotoa huduma hiyo, pamoja na Muunganiko wa Kimataifa wa Usimamizi waMambo ya Mafuta ya Ndege (JIG), ili kusambaza huduma bora zenye kiwango cha kimataifa katika maeneo anakonuia kutoa huduma.

Ismail anasema, kwa sasa wana uwezo wa kutunza lita milioni moja katika kiwanja cha KIA na lita milioni 18 katika bohari ya kampuni iliyopo Kigamboni, Dar es Salaam, zinazoweza kuongezeka baadae, kulingana na ongezeko la mahitaji, kutegemea namna biashara itakavyopanuka.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Julius Ndyamukama, anafafanua kuwa Lake Oil ni kati ya kampuni wazawa zilizokidhi vigezo vya kutoa huduma ya mafuta ya ndege.

Ndyamukama anatoa wito kwa kampuni zinazotoa huduma kwenye mamlaka za anga, kuendelea kujiimarisha kwa viwango vyenye ubora na kupambana katika masoko ya nje ya nchi, kama ilivyo hatua ya wazawa Lake Oil.

UKURASA 11

# Nipashe


Ijumaa Desemba 31, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580811

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## Ndugu makaburi yanayohamishwa Vingunguti wazidi

UKURASA 3

# Mapenzi yalivyo kiini cha ugonjwa wa akili

**DAKTARI** bingwa Muhimbili achambua ukubwa wa tatizo, wazee wasio na wenza vinara wa ubakaji... *Endelea ukurasa 2 & 10*



UKURASA WA 3

### NHC YAJA NA VITASA JANJA KUWABANA WADAIWA SUGU

MAJINA ya wadaiwa sugu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) yataanza kuanikwa hadharani kwenye vyombo vya habari Januari ...

UKURASA WA 4

### AJIRA 2,094 KUMWAGWA UJENZI RELI YA KISASA MWANZA - ISAKA

UJENZI wa reli ya kisasa kipande cha tano kutoka Mwanza hadi Isaka, Kahama mkoani...

UKURASA WA 4

### WAZIRI ATEMA CHECHE UCHAFU MASOKO DAR

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mazingira...



Wakazi wa jijini Dar es Salaam wakijiandikisha ili kupata chanjo ya corona, katika kituo cha daladala cha Feri jana, kwenye kampeni inayohamasishwa na Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA), kwa kushirikiana na Idara ya Afya Wilaya ya Ilala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Marufuku kuwavua samaki aina kasa visiwani Zanzibar

UKURASA 17

# Mbaroni akituhumiwa kuwa na picha za wafu

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA, DODOMA JIJI HAPATOSHI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mapenzi yalivyo kiini cha ugonjwa wa akili

**Na Daniel Limbe, CHATO**

LICHA ya jamii kutokuwa na uelewa wa magonjwa ya akili, mapenzi yametajwa kuwa moja ya sababu kubwa zinazochangia kuongezeka kwa tatizo hilo nchini.

Kwa mujibu wa Daktari Bingwa wa Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dk. Said Kuganda, jamii ina wagonjwa wengi wa afya ya akili ikilinganishwa na idadi inayofika kupata huduma kwenye vituo vya tiba.

Dk. Kuganda, akizungumza kwenye kipindi cha Meza Huru kinachorushwa na runinga ya ITV alisema, idadi ya kubwa ya wagonjwa wanaochanganyikiwa hutokana na kushindwa kukabiliana na hali ya tatizo ikiwamo kuachwa na mpenzi, kufiwa, madeni, umaskini uliopitiliza na wachache kuzaliwa na vinasaba vya ugonjwa.

Hata hivyo, alisema asilimia 80 ya magonjwa yote ya akili yanatibika na kupona kabisa, huku asilimia 15 yanatibika kwa kuendelea na dawa na asilimia 5 pekee huenda wasitibike kutokana na kurithi vinasaba vya ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu chini ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za kulevya, dawa zinazotumika nchini ni pamoja na heroin, mirungi, cocaine, petroli na gundi.

Licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na serikali kupambana na dawa za kulevya, jamii imeendelea kutumia bila kujali madhara makubwa yanayopatikana ikiwamo magonjwa ya akili, mimba zisizotarajiwa, magonjwa ya ngono pamoja na kupoteza kumbukumbu.

Madhara mengine ni uraibu, moyo, kifua kikuu, kusinyaa kwa mishipa ya damu hali inayosababisha shinikizo la damu, kiharusi, sonona, kukosa usingizi, saratani na hata vifo.

Dk. Peter Mfisi, Kamishna wa Kinga na Tiba kutoka mamlaka hiyo, ameiambia Nipashe kuwa matumizi ya bangi ni kichocheo kikubwa cha vijana kujidunga sindano wakiamini wanapunguza mawazo na baadhi yao kuwa na imani potofu za kuongeza akili za kufikiri.

"Licha ya changamoto zilizoko mamlaka yetu tunaendelea kutoa elimu kwa jamii, kudhibiti usambaaji wa dawa hizo pamoja na kutoa tiba kwa baadhi ya walioathirika na matumizi hayo," alisema Dk. Mfisi.

Takwimu toka kitengo cha kudhibiti dawa za kulevya mwaka 2020 zinaonyesha jumla ya waathirika wa afya ya akili 169,269 walipatiwa tiba kwenye hospitali mbalimbali nchini huku wanawake wakiwa ni 31,969 na wanaume 137,300.

Hassan Hoza na Titto Ibrahimu, wameishauri serikali kwa kushirikiana na wataalamu wa afya ya akili kutoa elimu kwa jamii ili kusaidia kupunguza tatizo hilo haraka, na kwamba lisipodhibitiwa mapema kipindi cha miaka 20 ijayo kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na kundi kubwa la jamii tegemezi kutokana na kupoteza uwezo wa kufanya kazi na vifo ambavyo vingeweza kuzuilika.

## Shule shikizi kuboreshwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesema serikali itahakikisha inazifikia shule shikizi zote zenye vigezo na kuzijenga ili kuwapatia fursa wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

Ummy Mwalimu aliyabainisha hayo jana kwenye ukurasa wake wa Instragram, akieleza namna serikali inavyotatua kero ya uhaba wa madarasa katika shule za msingi na sekondari.

Alisema kuwa huko nyuma watu hawakujali kuhusu shule au vituo shikizi, lakini serikali ya awamu ya sita imechukua hatua mahususi za kujenga madarasa ya kisasa 3,000 kwa mpigo katika shule shikizi 970.

Jana, Nipashe iliripoti kuhusu wanafunzi wa darasa la awali, la kwanza na pili katika kitongoji cha Imalange, kata ya Sabasabini, Halmashauri ya Ushetu, wanavyolazimika kusoma kwenye darasa lililojengwa kwa miti.

Darasa hilo ni shule shikizi ya Shule ya Msingi Kabanga ambayo wanafunzi hao hujiunga nayo wanapoingia darasa la tatu.

Akitumia ukurasa wa mbele wa gazeti la Nipashe toleo la jana lililokuwa na picha ya darasa hilo, Waziri Ummy alitoa ufafanuzi wake kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali kuboresha shule shikizi nchini.




Meneja wa Karakana Kuu ya TAZARA jijini Dar es Salaam, Jumanne Mnyawami (kushoto), akimwonyesha Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya moja ya mabehewa yaliyokarabatiwa kwenye karakana kuu ya TAZARA jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbaroni akituhumiwa kuwa na picha za wafu

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi limethibitisha linamshikilia Emanuel Pesa (37), mkazi wa Mbagala mkoani Dar es Salaam, kwa tuhuma za kukutwa na vitu mbalimbali vinavyoashiria uhalifu.

Inadaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alitiliwa shaka wakati wa ukaguzi kwenye Uwanja wa Ndege Mwanza Desemba 24, mwaka huu, alikotua majira ya saa 10:30 jioni alipokuwa anajiandaa kupanda ndege aina ya Airbus A220-300 ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwenda Dar es Salaam.

Inadaiwa kuwa baada ya kufika kwenye meza ya ukaguzi na kupekuliwa, alikutwa na kitambulisho ambacho ni mali ya Jeshi la Wananchi (JWTZ) chenye jina YA P 9100 CA NYANDA namba GF6872, ambapo wakati wa mahojiano aldidai ni cha kaka yake.

Vitu vingine anavyodaiwa kukutwa navyo mtuhumiwa huyo ni noti za Msumbiji MZN 200 (sawa na Sh. 7,127.75) pamoja na simu mbili, ambazo inasemekana zilipopekuliwa, zilikutwa na picha za watu waliofariki dunia katika matukio ya mauaji, zikiwamo za wanawake na watoto, zote zikidaiwa zilipigwa siku za karibuni.

Kamanda wa Polisi Viwanja vya Ndege, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi Jeremiah Shila, alisema kuwa baada ya kukaguliwa, mtuhumiwa huyo alipelekwa Kituo cha Polisi Mwanza.

"Mara kwa mara tumekuwa tukisisitiza abiria kuwa ni muhimu kuhakikisha wanakagua mabegi yao vizuri na kujiridhisha kabla ya kutoka nyumbani ili kuepuka usumbufu, ulinzi umeimarika, hakuna kitu chochote ambacho ni kinyume cha sheria kitaruhusiwa kupita," alisema.

Kamanda Shila alikumbusha kuwa wapo watu waliopata matatizo kutokana na kushika mabegi ya watu bila kujihakikishia kuwa ni salama, akitoa wito kwa abiria kuhakikisha wanaepuka tabia ya kukubali kushika mizigo ya watu wasiowajua.

"Kuna watu wanabeba vitu ambavyo sio salama, akijua kuwa polisi wanamfuatilia anaamua kumwachia mwingine. Watu wawe makini na hilo. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine wa usalama tumejipanga vizuri kudhibiti uhalifu na katika viwanja vyote kutakuwa na ukaguzi maalumu," alionya.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'azi, alithibitisha wanamshikilia mtuhumiwa huyo na wanaendelea na upelelezi.

"Mpaka sasa mtuhumiwa yuko mikononi mwa vyombo vyetu vya usalama akifuatiliwa mtandao wake.

Baada ya siku chache, upelelezi utakamilika, tunatoa taarifa kamili," Kamanda Ng'azi alisema.

## HABARI KITAIFA

# Kimei: Tanzania si wa kwanza kukopa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MBUNGE wa Vunjo, Dk. Charles Kimei, amesema Tanzania si nchi ya kwanza na wala haitakuwa ya mwisho kutekeleza miradi kwa kukopa.

Katika hafla ya kupokea vyumba vya madarasa 85 vilivyojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.7, mbunge huyo alisema juzi kuwa serikali ina nia ya dhati katika kuwaletea wananchi wake maendeleo hususani kwa wale wa ngazi ya chini, lakini wapo baadhi ya watu wenye maneno ya kukatisha tamaa, hivyo wasipewe nafasi.

Alisema Deni la Taifa bado ni himilivu na kuwa si tishio kama ambavyo inasemekana. Alisema nchi nyingi duniani zimekuwa zikikopa ili kujenga miundombinu ambayo itawawezesha wananchi wake kufanya biashara sambamba na kutoa huduma mbalimbali.

Kwa mujibu wa mbunge huyo ambaye ni mtaalamu wa uchumi, bado Tanzania ina sifa za kukopesheka na ndio maana imeendelea kuaminiwa na wahisani mbalimbali ikiwamo Mfuko wa Fedha Duniani na Benki ya Dunia (WB).

"Sisi bado tupo katika hali nzuri ya kukopesheka na ndio maana Rais Samia Suluhu Hassan alivyoenda kukopa, aliaminiwa mara moja tofauti labda na mataifa mengine, sisi bado tunayo rekodi nzuri katika mkopo na suala la mkopo si aibu, hatujaanza sisi kukopa wala hatutakuwa wa mwisho," alisema.

Alisema yeye kama mtaalamu wa fedha, alishawahi kuzunguka katika taasisi nyingi na kujifunza vigezo vya kupewa mkopo na kuwa ni lazima uwe na rekodi nzuri ya matumizi ya mkopo lakini pia kipaumbele cha mkopo wenyewe kitambulike au kuonekana.

Alisema fedha hizo zimeleta mabadiliko makubwa kwa muda mfupi, hivyo wananchi waunge jitihada za miradi hiyo pamoja na inayoanzishwa na serikali hususan katika ile miradi ambayo inamgusa moja kwa moja mwananchi wa chini.

"Serikali imekuwa ikianzisha miradi ambayo imekuwa ikigusa wananchi wa hali ya chini ikiwamo maji, barabara na afya hivyo wananchi hawana budi kuunga mkono na kuachana na propaganda zinazotolewa na baadhi ya wanasiasa wasio iwazia mema nchi dhidi ya miradi hiyo" alisema Dk. Kimei.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abbas Kayanda, alisema ifikapo mwezi Januari mwakani, yaani kuanzia kesho, mzazi ambaye hatampeleka mtoto shule atakumbana na mkono wa sheria.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya TICTS inayojishughulisha na makontena Tanzania katika Bandari ya Dar es Salaam, Horace Hui (kushoto), akiwa na Mkurugenzi wa Maendeleo wa kampuni ya hiyo, Donald Talawa, wakishiriki kufanya usafi katika fukwe ya Coco, jijini jana, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono serikali kufanya usafi katika mazingira yanawazunguka wananchi kupitia kampeni ya "GO Green" kwa kushirikiana na uongozi wa Serikali ya Mtaa wa Oysterbay. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndugu makaburi yanayohamishwa waongezeka

**Na Maulid Mmbaga**

OFISA Afya wa Jiji la Dar es Salaam, Reginald Mlay, amesema kuwa uhamishaji makaburi yaliyopo pembezoni mwa Mto Msimbazi, Kata ya Vingunguti, umekuwa na changamoto baada ya kuongezeka kwa ndugu wanaotaka miili ya ndugu zao ihamishwe.

Alisema idadi ya awali iliyopangwa kuhamishwa ni 200, lakini hadi sasa wanaona itafika zaidi kwa kuwa ndugu wengi wanajitokeza kutaka mabaki ya miili ya wapendwa wao ihamishwe.

Makaburi hayo ni yaliyopo umbali wa mita 10 kutoka Mto Msimbazi kutokana na baadhi kuzolewa na kuyahamishia Mwanagati, Kata ya Kitunda, kazi iliyoanza Desemba 27, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe, Mlay alisema ongezeko hilo limetokana na baadhi ya ndugu kuchelewa kujiandikisha wakidai wengi walikuwa wakijiandikisha wakati zoezi likiendelea.

"Hiyo imekuwa ni changamoto kwetu, lakini kuna baadhi ya makaburi ambayo yalikuwa hayana alama, yalikuwa hayaonekani vizuri na kwenye hesabu zetu za mwanzo hayakuweza kuhesabiwa mtu anakuja anakuambia mimi nilizika hapa ukichimba unakuta kweli mabaki ya mwili yapo," alisema.

"Imekuwa ni changamoto kwani tumepata makaburi mengi kuliko tulivyokuwa tunatarajia tumewajulisha viongozi wa halmashauri na tutafanya utaratibu pengine tutaongeza siku mbili au tatu ili tuweze kukamilisha suala hili hasa katika lile eneo ambalo ni hatarishi," alisema Mlay.

Aliongeza kuwa katika hatua hiyo kuna baadhi ya ndugu wa marehemu ambao walitaka wasafirishe ndugu zao wakazike tofauti na eneo lililotengwa wawapeleke mikoani na tayari wameshawaandalia vibali akiwataka wengine wanaotaka kusafirisha kutoa taarifa mapema.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Butiama, Kata ya Vingunguti, Nimzihirwa Mjema, alisema mpaka sasa suala la kuhamisha makaburi ambayo yako katika hatari ya kusombwa na mafuriko ya maji ya Mto Msimbazi linaendelea vizuri.

"Hadi sasa tumefanikiwa kuhamisha zaidi ya mabaki ya miili 138 na leo (jana' bado tunaendelea tunategemea kupata miili zaidi ya 60 na bado kuna mingine ambayo imebaki na tunategemea serikali ya halmashauri ya jiji itaendelea kuiondoa ili hii changamoto isiendelee kuonekana katika eneo hili," alisema Mjema.

Pia aliwataka wananchi wa eneo hilo kuwazuia watoto wao wasicheze katika eneo la makaburi na pembezoni mwa kingo za mto huo.

Mmoja wa ndugu wa marehemu aliyezikwa eneo hilo, Josefu Boniface, alisema makaburi mengi yalisombwa na maji na aliishukuru serikali kwa uamuzi wa kuhamisha yaliyobaki kwa kuwa inawarahisishia kupunguza gharama za kuhamisha.

"Tunashukuru kwa taratibu zilizofanyika katika kipindi hiki kutolewa ndugu zetu hata mimi nimetoa mabaki ya mwili wa mwanangu leo hii (jana) yamepelekwa Mwanagati, tunaishukuru serikali kwa kuokoa jahazi hili kwasababu mmong'onyoko unazidi kuendelea na wengi wameondoka," alisema Boniface.

# NHC yaja na vitasa janja kuwabana wadaiwa sugu

**Na Elizabeth Zaya**

MAJINA ya wadaiwa sugu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) yataanza kuanikwa hadharani kwenye vyombo vya habari Januari mwakani.

Vilevile, uongozi wa shirika hilo umesema Sh. bilioni 26 linazozidai kwa sasa zinatosha kujenga nyumba mpya 450, huku likibuni njia mpya ya kuwabana wapangaji wake kwa kuwa na vitasa janja vinavyoifunga nyumba pale mpangaji anaposhindwa kuilipia.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Uhusiano wa Shirika hilo, Muungano Saguya, alisema tayari wameandaa mpango kabambe wa kukusanya kodi zake zote ambazo linadai ambao utaanza rasmi Januari.

Alisema wadaiwa wa shirika hilo wako wa aina mbili, ambao bado wanaishi kwenye nyumba hizo na waliokwishahama.

Meneja huyo alisema shirika hilo linadai malimbikizo ya madeni ya Sh. bilioni 26 kutoka kwa wapangaji wake na tayari limeanza kufanyia mapitio madeni hayo kwa kuyahakiki.

"Lengo ni kubainisha kila mdaiwa na mahali alipo, anadaiwa kiasi gani ili mwezi ujao shirika lianze kampeni kabambe ya kukusanya madeni hayo," alisema.

Meneja huyo alisema malimbikizo ya madeni hayo yakikusanywa, yatasaidia kujenga nyumba 450 na katika mpango wao huo watahakikisha madeni yote yanakusanywa.

"Na katika mpango huu kambambe wa kudai madeni, hatua mbalimbali zitachukuliwa ikiwamo kuwatangaza hadharani kwenye vyombo vya habari pamoja na kuwafikisha mahakamani wadaiwa," alisema.

Saguya alisema mpango mwingine mkakati wa kiteknolojia ambao shirika hilo limekuja nao katika kudhibiti wadaiwa kwenye nyumba zake, ni wa kuzifunga nyumba za wadaiwa moja kwa moja na hawataweza kuingia ndani wanapokuwa wanadaiwa.

"Shirika limebuni teknolojia mpya ya vitasa janja (smart lock) vitakavyofungwa katika nyumba kadhaa za mfano, ambavyo vitasaidia kuwabana walimbikizaji madeni sugu na hivi vitasa vitakuwa vinaifunga nyumba automatically inapokuwa inadaiwa. Kwa hiyo, mhusika hawezi kuingia mpaka alipe," alisema Saguya.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa Miliki na Masoko wa Shirika hilo, Elias Msese, alisema wengi waliolimbikiza madeni katika nyumba zao ni wafanyabiashara ambao wengi wao walifunga biashara zao na kuhama kwenye nyumba hizo baada ya kuathiriwa na virusi vya corona vinavyosababishwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu, maarufu UVIKO-19.

"Ni kweli baadhi ya taasisi za serikali zilikuwapo kwenye nyumba zetu na zikahama, lakini deni lao halikuwa kubwa, lilikuwa Sh. bilioni 5.5 na mpaka sasa Sh. bilioni tatu zimelipwa na hiyo, zilizobaki zinatarajiwa kumaliziwa wakati wowote. Kwa hiyo, asilimia kubwa ya wadaiwa wetu ni wafanyabiashara," alisema Msese.

Pia alibainisha kuwa tayari miradi yote 26 ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu imekamilika na mipango iliyopo kwa mwaka ujao ni kufanikisha miradi mingine mikubwa minne ikiwamo ya Morocco Square, Kawe 711, Golden Premier Residence (GPR) pamoja na Plot 300 Regent Estate ambayo ilisimama tangu mwaka 2017 kutokana na upungufu wa fedha.

HABARI KITAIFA

# Ajira 2,094 kumwagwa ujenzi reli ya kisasa Mwanza- Isaka

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

UJENZI wa reli ya kisasa kipande cha tano kutoka Mwanza hadi Isaka, Kahama mkoani Shinyanga, chenye urefu wa kilometa 341, umeajiri Watanzania 2,094 na vibarua 859.

Naibu Meneja wa Mradi huo Mhandisi Alex Bunzu, alibainisha hayo jana wakati akisoma taarifa ya utekelezaji kwenye kikao cha Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, kutoka katika taasisi mbalimbali. Alisema mradi huo wa reli ya kisasa umeshaanza kutekelezwa kwa gharama ya Sh. trilioni 3.062 na ulitiwa saini Januari, mwaka huu, na unatarajiwa kukamilika mwaka 2024 na kwamba Watanzania wataendelea kunufaika hatimaye kujikwamua kiuchumi.

"Mradi huu wa reli ya kisasa (SGR) umezingatia utoaji wa ajira kwa Watanzania, wakiwamo vijana waliohitimu elimu ya juu na ufundi pamoja na kutoa kazi kwa kampuni za ndani 32 zenye thamani ya Sh. bilioni 14.3," alisema Bunzu.

Pia alisema katika ulipaji fidia kwenye maeneo ya watu ambao ardhi zao zimetwaliwa, Sh. bilioni 5.3 zimeshaidhinishwa kwa ajili ya kazi hizo.

Mbunge Katambi alipongeza mradi huo kutoa kipaumbele kuajiri Watanzania pamoja na wazawa ambao wanapitiwa na mradi huo. Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, alisisitiza pia kwenye mradi huo yazingatiwe masuala ya kampuni kuwajibika kwa jamii (CSR) kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kuacha alama. Katika hatua nyingine, Katambi aliziagiza taasisi mbalimbali za serikali mkoani Shinyanga, kila moja itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwahudumia wananchi na si kusubiri kufanya kazi kwa kusukumwa. Naye Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) Mkoa wa Shinyanga, Richard Mpongo, alishauri serikali katika utoaji ajira kwenye mradi huo watu wenye ulemavu wapewe ajira kwa mujibu wa sheria.



Wafanyabiashara wadogo wakipanga viatu pembeni mwa barabara ya Morogoro, Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam. Hata hivyo, hawatakiwi kuwapo eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waziri atema cheche uchafu masoko Dar

**Na Gwamaka Alipipi**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Mazingira, Hamad Hassan Chande, ameziagiza halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam kutafuta makandarasi wenye uwezo wa kuzoa taka katika masoko.

Pia ameziagiza halmashauri kuhakikisha zinatafuta makandarasi walio tayari kuwekeza kwenye masoko kwa kufuata mikataba inayoingia.

Alitoa agizo hilo jana Dar es Salaam baada ya kufanya ziara ya ukaguzi katika soko la Tegeta Nyuki na kukuta hali ya usafi katika soko hilo si nzuri, huku vizimba vya kuhifadhia taka vikiwa vimejaa uchafu.

"Tafuteni makandarasi wengine kama hawa hawafai. Tafuteni walio tayari kuwekeza. Makandarasi tutakaowapa mkataba wawe tayari kuondoa taka kama walivyokubali kwenye mkataba," alisema Chande.

Akitoa ufafanuzi wa hali ya usafi katika masoko, Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, Awadhi Jambo, alisema: "Tumeweka mkakati wa kukarabati masoko yote yaliyopo katika halmashauri na kuna fungu limetengwa.

Kwa soko la Tegeta Nyuki tunataka kulijenga upya".

Naibu Waziri Chande, alifanya ziara ya kushtukiza katika kiwanda cha kuzalisha malighafi za kutengenezea magunia kitwacho H&J Fibre Investment na kutoa siku 14 kwa uongozi kufanya marekebisho ya miundombinu ya majitaka.

"Kiwanda hakijafuata sheria za mazingira, usalama wa wafanyakazi na wakazi wanaozunguka kiwanda upo hatarini, maji yenye kemikali yanatiririka. Sasa natoa siku 14 wahakikishe wanarekebisha miundombinu ya majitaka, vinginevyo tutachukua hatua kali zaidi," alisema Chande.

Naye Mhaidolojia kutoka Bonde la Mto Wami Ruvu, Nestory Lucas, alisema kuna taka za sumu nyingi zimeelekezwa kwenye Mto Ng'ombe, hivyo ni kosa kisheria na mmiliki wa kiwanda afike ofisini apewe utaratibu wa namna ya kutupa maji kwenye mto.

Kaimu Meneja wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Lilian John, alisema kiwanda hicho kina mifuko mingi yenye kemikali na maji machafu.

Alisema wafanyakazi wake hawana vitendea kazi vya kujizuia na magonjwa mbalimbali, wamekiuka kanuni za afya ya mazingira na hawana ofisa mazingira.

Akitoa utetezi wa hoja hizo, Meneja Uendeshaji wa Kiwanda hicho, Kelvin Payovela, alisema wameyapokea maagizo na wanamhakikishia ndani ya muda aliotoa watakuwa wametekeleza baadhi ya maagizo ikiwamo vitendea kazi kwa wafanyakazi.

"Lakini hili la utiririshaji wa maji taka litachukua muda kidogo kwa sababu lina mlolongo na si la siku moja," alisema.

# Kero ya wanafunzi kutembea umbali mrefu yatatuliwa

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

WANAFUNZI 225 wa Kata ya Rukoma wilayani Bukoba waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani, wataondokana na adha ya kutembea umbali kati ya kilometa saba hadi 18 kwenda Shule ya Sekondari Rubale.

Hatua hiyo inatokana na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba kuanza ukamilishaji wa usajili wa shule mpya ya kata hiyo, ambayo baadhi ya madarasa yake yamejengwa kwa fedha za UVIKO - 19.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na Diwani wa Rukoma na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Musrhid Ngeze, Ofisa Elimu wa Kata hiyo, Dunkan Byobangila, alisema katika fedha za UVIKO - 19, walipata Sh. milioni 60 kwa ajili ya kujenga vyumba vitatu vya madarasa na kutengeneza madawati 150.

Byobangila alisema pia wananchi walijitolea nguvu zao na kuchanga Sh. milioni 42 na halmashauri ikatoa Sh. milioni 25, hivyo kufikisha Sh. milioni 67 zilizotumika kujenga vyumba vingine vitatu. Alisema hatua hiyo imefanya shule hiyo mpya kuwa na vyumba sita vya madarasa.

"Katika shule sita za msingi zilizoko katika kata hii, watahiniwa waliofanya mtihani wa kuhitimu darasa la saba mwaka huu walikuwa 295. Kati ya hao, 225 walifaulu na tunatarajia wajiunge na kidato cha kwanza katika shule hii mpya. Wanafunzi hawa waliofaulu katika kata ya Rukoma ni sawa na asilimia 85 ya waliofanya mtihani," alisema.

Naye Ngeze alisema yeye na mkurugenzi mtendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo watakamilisha usajili wa shule hiyo, ili Januari watoto wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika kata hiyo, waanze masomo.

"Kwa sababu sasa madarasa yapo na mchakato wa kukamilisha usajili unaendelea, hakuna tena haja ya watoto kuwaacha wateseke kwenda Shule ya Sekondari Rubale. Tutahakikisha Januari wote wanaanza masomo hapa Rukoma. Nawaahidi hilo," alisema Ngeze.

Pia alisema wamepata Sh. milioni 470 kwa ajili ya kujenga madarasa mengine manane, jengo la utawala, maabara tatu na matundu 20 ya vyoo katika shule hiyo na kwamba kufikia Februari, mwakani, vitu vyote hivyo vitakuwa vimekamilika na kuwezesha kuwapo kwa madarasa ya kutosha.

Mmoja wa wananchi walioshiriki mkutano huo, Hidaya Omary, alisema watoto wao waliteseka muda mrefu kwenda kufuata elimu mbali na kata yao na kwamba wamepata faraja kujengewa shule karibu na hawakulitarajia hilo.

Mwananchi mwingine, Najiath Shaban, alisema mbali na watoto wa kike kubeba mimba na wengine wa kiume kuacha shule kutokana na umbali, pia baadhi ya wazazi waliwalazimisha watoto wao wafanye vibaya katika mitihani ya kuhitimu darasa la saba ili wasiendelee na masomo ya sekondari.

"Kutokana na umbali mrefu, kuna baadhi ya wazazi waliwaambia watoto wao wasifanye vizuri katika mitihani hata kama walikuwa na akili. Walitii wazazi wao na hii ilitokana na kwamba shule wanakopelekwa ni mbali mno na wazazi hawana fedha kwa ajili ya kuwanunulia watoto baiskeli," alisema.

**HABARI KITAIFA**

# Korti Kuu yabariki mnada deni bil. 1/-

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekataa kuizuia Benki ya Biashara Tanzania Limited na wenzake kuuza kiwanja cha Kampuni ya Leopard Net Logistics Limited kwa kushindwa kulipa mkopo zaidi ya Sh. bilioni moja baada ya kuona maombi hayo hayana mashiko.

Uamuzi huo ulitolewa juzi mbele ya Jaji Juliana Masabo baada ya kupitia hoja za mlalamikaji na walalamikiwa katika maombi hayo.

Kampuni ya Leopard iliwasilisha maombi dhidi ya mlalamikiwa wa kwanza, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania, wa pili Wakala wa Misitu Tanzania, watatu Kampuni ya Afrimax Limited na mlalamikiwa wa nne, Mwanasheria wa Serikali.

Katika maombi hayo, mlalamikaji alikuwa akiwakilishwa na Wakili Elly Msyangi na walalamikiwa wakiwakilishwa na Daniel Nyakiha.

Mlalamikaji kupitia wakili wake, Msyangi aliomba mahakama itoe zuio la muda la kuuzwa kwa kiwanja chake namba 67 H2 FLUR III kilichoko maeneo ya Temeke Dar es Salaam alichoweka dhamana benki kwa ajili ya kupata mkopo.

Katika maombi yake, aliambatanisha kiapo kilichoapwa na Nabii Juma Rashid ambaye ni Ofisa Mkuu wa Kampuni ya Leopard.

Inadaiwa mkataba ulikuwa wa kuvuna bidhaa zote za misitu na kukusanya katika mradi wa Hydropower ulioko Rufiji.

Mkataba kati ya mlalamikaji na mlalamikiwa wa pili, Wakala wa Misitu uliingiwa Desemba 20, mwaka 2018. Katika mkataba huo, inadaiwa mlalamikiwa wa pili aliridhia mlalamikaji kuvuna miti aina zote iliyokuwapo block namba tatu na nne ambayo ni sawa na ekari 6,000 zenye mita za mraba 207,000.

Mlalamikaji anadai baada ya mkataba huo, aliomba mkopo benki kwa ajili ya kuongeza mtaji wa kufanya kazi hiyo jumla ya Sh. bilioni 1.1 na kwamba alivuna mita za mraba 2,000 tu maeneo mengine hayakuwa na miti bali majani.

Alitakiwa hadi Juni 22, mwaka huu awe amelipa mkopo huo, lakini alishindwa, akapewa notisi ya kushinikizwa kulipa Sh. 1,331,957,588.56 (biloni 1.332) ndani ya siku 60 na akishindwa, mali yake inauzwa.

Novemba mwaka huu, alipewa notisi nyingine kupitia mlalamikiwa namba tatu, akishinikizwa kulipa deni ndani ya siku 14.

Mlalamikaji aliwasilisha notisi ya siku 90, akiomba kuishtaki serikali na kwa kuhofia kuuzwa kwa eneo lake na aliwasilisha maombi ya zuio la muda. Alidai notisi ya kuishtaki serikali inaisha Februari 9, mwakani na anaomba mahakama ikubali maombi yake na itoe zuio. Akijibu hoja hizo, Wakili wa Walalamikiwa, Nyakiha, alidai mkataba kati ya mlalamikaji na mlalamikiwa namba mbili ulifika mwisho Februari mwaka 2019, hivyo kwa sasa hawana mkataba wowote.

Anadai mlalamikiwa namba mbili alitoa muda wa nyongeza kwa mlalamikaji kukusanya vifaa vyake na miti iliyobakia katika eneo la mradi. Anadai mlalamikaji kashindwa kulipa mkopo mwaka mzima na hakuwahi kulipa hata rejesho moja wakati alikuwa akiendelea na biashara na kupata faida huku mlalamikiwa namba moja akipata hasara.

"Kama mahakama itakubali maombi ya mlalamikaji, mlalamikiwa namba moja hatalipwa fedha anazodai," alidai Nyakiha na kuomba maombi yakataliwe.

Katika uamuzi wa mahakama, Jaji Masabo alisema baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, imeona kwamba mlalamikaji habishi kwamba anadaiwa na aliweka dhamana ya kiwanja.

Jaji Masabo alisema kazi ya mahakama ni kutoa haki kwa pande zote mbili, hivyo baada ya kupitia hoja, iliona maombi ya mlalamikaji ya zuio hayana mashiko, hivyo inayatupilia mbali.



Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, akizungumza na wanachama wa chama hicho katika kijiji cha Mikangaula Jimbo la Lulindi, mkoani Mtwara juzi, alipokuwa kwenye ziara ya kuimarisha chama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Viongozi wa wilaya lawamani migogoro wakulima, wafugaji

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WAKULIMA wa Kijiji cha Itete wilayani Malinyi, wameilalamikia serikali ya wilaya kutosikiliza kilio chao cha muda mrefu juu ya baadhi ya wafugaji kulisha mifugo katika mashamba yao.

Jambo hilo, wamesema limesababisha kuzuka kwa mapigano ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji, hivyo kusababisha kifo cha mtu mmoja.

Wakizungumza juzi katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Malinyi, Antipas Mgungusi, baadhi ya wanakijiji hao walisema kero hiyo ya muda mrefu ya mifugo kuingia mashambani imekuwa sugu.

Castory Kisawiki, mmoja wa majeruhi katika tukio la mapigano lililotokea Desemba 27, mwaka huu, alisema kijiji hicho kimezungukwa na wafugaji jamii ya Waisukuma ambao wamekuwa wakifanya vitendo hivyo kwa makusudi na hata wakijaribu kuwazuia, wanaishia kushambuliwa kwa mapanga na virungu.

"Tunaomba serikali kuu itusaidie kwa sababu hawa wafugaji wanatunyanyasa sana na wilaya imeshindwa kutusaidia. Malalamiko yetu wanayo muda mrefu na hata marehemu Abdul ameuawa kwa sababu walikuja kunisaidia mimi shambani kwangu baada ya kuwapa taarifa kuwa nimevamiwa na kundi la ng'ombe," alisema.

Naye Mzee Mwigulu Sadam, ambaye anatoka katika jamii ya wafugaji, akizungumza huku akibubujikwa na machozi, alisema tukio hilo limesababisha yeye na familia yake kukosa makazi huku tani tatu za mazao yake zikiteketezwa kwa moto.

Alisema familia yake inawatoto 24 na wake wawili walikuwa wakiishi vizuri na jamii ya wakulima kwa kuwa nao shughuli yao kubwa ilikuwa ni kilimo lakini hali iliyotokea, watu hao hawakujali chochote na kuchoma nyumba za waliohusika na wasiohusika.

"Mimi naishi hapa na wake zangu na watoto na tunashirikiana vizuri tu na wakulima wa hapa. Wanaofanya vitendo vya kulisha mashambani ni wafugaji walioko upande wa pili kule, lakini bila kujali, wamechoma hadi kwangu. Naomba serikali inisaidie kwa sababu sasa hivi mpunga wote umechomwa ndani ya nyumba," alisema Sadam.

Mbunge Mgungusi alikiri kupokea malalamiko hayo na kuahidi kuyafikisha katika ngazi za juu ili hatua zaidi zichukuliwe na kukomesha kabisa migogoro ya wakulima na wafugaji.

Alisema migogoro iko katika maeneo mengi wilayani hapa na kuwataka wanakijiji kuwa watulivu wakati vyombo vya dola vinaendelea na uchunguzi wa matukio hayo ili hatua za kisheria zichukuliwe.

"Wengi wametoa malalamiko yao kuhusiana na jambo hili na kuonyesha kwamba hawakuwahi kuona jitihada za makusudi za serikali ya wilaya za kusaidia. Kimsingi tatizo lipo wilaya nzima si Itete peke yake, kwa hiyo nikiwa kiongozi wa kisiasa, watu wote ni wangu nitalichukua hili na kufikisha panapohusika," alisema Mgungusi.

# Wajawazito walia ukosefu zahanati

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WAJAWAZITO katika kijiji cha Mkwanga wilayani Kigoma wanapata adha wakati wa kujifungua kutokana na kijiji kutokuwa na zahanati hali ambayo inachangia kuwapo vifo vya mama na mtoto.

Kijiji hicho kisicho na zahanati kiko katika kata ya Mkongoro ambayo pia haina kituo cha afya, hivyo wajawazito hulazimika kusafirishwa kwa pikipiki kwenda Kituo cha Afya cha Bitale katika kata ya Bitale.

Upendo Jonas, mkazi wa kijiji hicho, alisema mwaka 2020 binti yake alipokuwa na ujauzito wa kwanza, mtoto alifia tumboni kutokana na kuchelewa kupata huduma za afya katika Kituo cha Afya Bitale baada ya kuhangaika muda mrefu kutafuta usafiri .

"Binti yangu alipoteza mtoto, yaani tulihangaika namna ya kutafuta pikipiki na hadi tunafika kituo cha afya wakakuta mtoto amefia tumboni," alisema.

Naye Amina Bahita alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha wajawazito kuteseka hasa namna ya kusafirishwa hadi ziliko huduma husika, hivyo kuiomba serikali kuchukua hatua za haraka zitakazosaidia kuongeza usalama kwa mama na mtoto.

Mwenyekiti wa kijiji cha Mkwanga, Paulo Ntibalio, alisema hawana zahanati kutokana na kukosa eneo la kujenga na wameanza mchakato wa kukusanya fedha zitakazowezesha kununua eneo .

"Maeneo yote ni ya watu na hakuna aliye tayari kutoa. Tunaendelea na taratibu za kupata eneo japo lipo eneo moja tumepata la Sh. milioni 12 ambalo kama kijiji hatuna uwezo wa kupata fedha hizo," alisema.

Diwani wa Mkongoro, Maliki Makunda, alisema anasubiri serikali ya kijiji ikamilishe kupata eneo kisha waanzishe michango ya kuinua boma na kwenda kuomba fedha serikalini ili kukamilisha.

Kuhusu kituo cha afya, Makunda alisema tayari eneo limepatikana katika kijiji cha Mkongoro na baadhi ya vitendea kazi kama mawe, matofali na mchanga vipo ila kinachosubiriwa ni uongozi wa halmashauri kwenda kupima baada ya sikukuu kupita na hatimaye kuruhusu ujenzi uanze.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tuuanze 2022 kwa nguvu mpya kukabili changamoto

**IMEBAKI** siku moja kumaliza mwaka 2021 na kuingia 2022, huku kila aliyefanikiwa kuvuka akianza mwaka mpya kwa tumaini jipya, malengo na mikakati aliyojipangia.

Wengi huanza mwaka mpya kwenye nyumba za ibada kumwomba Mungu awaongoze wawe na mwaka mpya wenye mafanikio na kutimiza malengo waliyojiwekea, amani na ushindi kwenye nyanja mbalimbali za maisha.

Mwaka 2021 kama ulivyokuwa mwaka 2020 ulijaa na changamoto kubwa ya UVIKO-19, ugonjwa ambao umebadilisha muundo wa maisha kuanzia namna watu walivyokuwa wakiishi na kusafiri.

Aidha, uchumi wa dunia, nchi na mtu mmoja mmoja umetikiswa kwa kiasi kikubwa kwa kuwa watu walifilisika, zipo sekta zilizoathiriwa kama ya utalii ambayo hutegemea wageni kutoka mataifa mbalimbali kutembelea ili kupata fedha za kigeni.

UVUKO-19 tutaendelea kuishi nayo kama magojwa mengine na ndiyo maana ni muhimu kutafuta namna ya kuendelea kuishi na kufanya shughuli za uzalishaji kama kawaida ili maisha yaendelee.

Ni muhimu kila mmoja kuhakikisha anachanjwa kwa kuwa faida ni nyingi na kubwa, lakini kuendelea kujikinga na UVIKO-19, pamoja na kuhakikisha maisha yanaendelea kwa kufanyakazi kwa bidii. Muhimu kuukaribisha mwaka 2022 kwa amani, ibada na matumaini mapya huku kila mmoja akiweka mikakati ya kufikia malengo ya kubadili maisha yake kutoka hatua moja kwenda nyingine.

Kama taifa tunapaswa kuangalia changamoto kubwa zilizoko na kuwa na mikakati ya kuzitatua kwa kuhakikisha tunabaki na taifa moja lenye mshikamano na upendo mkubwa.

Mathalani, kuna mambo kiporo ambayo ni mjadala mkubwa kwa taifa na sasa tunavuka nayo mwaka 2021, ambayo ni kilio cha Katiba mpya hasa kufanya marekebisho kwenye mambo ya msingi likiwamo takwa la kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi, mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, malalamiko ya majeraha kwa walioteswa, waliodhulumiwa, walioporwa na kuumizwa kiasi cha kutaka tume ya uchunguzi ya kijaji.

Mengine ni baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa na wafuasi vya upinzani kukamatwa, sheria mbalimbali ikiwamo ya tozo, ufujaji wa fedha za umma ambazo hujitokeza kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG).

Mengine ni uwajibikaji wa watumishi wa umma kwamba ile hali ya kufanyakazi kwa mazoea na sio kwa bidii kama inavyotakiwa, ili kuendelea kuwahudumia wananchi ambao ndiyo wenye serikali na wanalipa kodi.


Lazima kuwe na bidii binafsi katika kutekeleza majukumu ya kila siku ili kuwa na uzalishaji wa juu, kuhakikisha wananchi wanapata huduma stahiki kuanzia kwenye ofisi za ngazi ya kijiji au mtaa, hospitalini na kwingine ambako ni muhimu.

Mwaka 2022 uwe wa mabadiliko makubwa kuanzia kwa mtu binafsi na taifa kwa ujumla, ikiwa kila mmoja atawajibika uzalishaji utaongezeka na uchumi utazidi kustawi.

Katika kufanya yote hayo ni muhimu kulinda amani, utulivu na umoja wa taifa, kwamba pamoja na tofauti za dini, itikadi za kisiasa na hali za maisha bado tunaendelea kuwa wamoja tunalilinda taifa kwa wivu mkubwa.

Nchi hujengwa kwa ushirikiano baina ya waliopewa mamlaka na walipakodi, ni muhimu kuimarisha ushirikiano huo ili kulinda nchi kuanzia kwenye kitongoji, mitaa hadi taifa kwa kuwa wahalifu na wala rushwa ni miongoni mwa wana jamii na sote tuna wajibu wa kuwatengeneza kuwa raia wema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




# Muungwana Lazima Nilonge



## Jamani TARURA mnavyotumika ni mtihani kwetu wananchi

Na Anthony Gervas, MWANZA

**LEO** nageuza macho yangu katika miundombinu ya barabara zinazojengwa kupitia Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), ambazo zinageuka kuwa kero kubwa kwa wananchi katika baadhi ya halmashauri za wilaya mbalimbali nchini, kutokana na kujengwa chini ya kiwango kinachotakiwa na serikali.

Barabara hizo zilizoko mijini na vijijini, awali zilikuwa zikisimamiwa na halmashauri zenyewe, lakini baadaye serikali ikaanzisha TARURA na kuipa mamlaka ya kuzisimamia, ili kuepuka 'upigaji' fedha za miradi hiyo unaodaiwa kufanywa na watumishi na watendaji ngazi za vijiji, hata kata hali ambayo ni kinyume cha sheria.

Pamoja na lengo zuri la serikali kufanya mabadiliko hayo, ikikerwa na tabia ya 'upigaji' pesa za umma kienyeji, bado ninaona ishara ya mapengo mahali fulani.

Najua ni maneno yanayoweza kuwakera wasimamizi wa miradi hiyo TARURA katika maeneo fulani, lakini ukweli ndiyo huo mimi nasema kile ninachokiona kwa kukishuhudia hasa vijijini, barabara nyingi zinabaki kero kubwa kwa wananchi, hata madiwani wa baadhi ya halmashauri za wilaya wamekuwa wakilazimika kulalamika katika vikao vyao vya mabaraza.

Barabara nyingi zinaharibika kwa muda mfupi na kushindwa kupitika mara baada ya kumaliza kujengwa, makaravati, madaraja nayo yanakuwa hayaeleweki, siyo imara, mengi hukatika na kuziba sehemu husika ya kupitisha maji.

Nauliza wahusika wa TARURA, hususani meneja wake wanaosimamia miradi hiyo, naamini kwa hili, sidhani serikali inapaswa iwapeleke kusoma tena darasani, ndipo mrudi kufanya kazi nzuri. Au nanyi mmeona ni sehemu ya uhondo wenu katika mazingira hayo tata?

**TARURA iko nchi nzima. Hapo niseme, kulikoni halmashauri zingine zinafanya vizuri. Mkikaguliwa, naamini baadhi ya maeneo mna maandiko bora kujieleza, lakini haifanani na kilichoko penye ushuhuda. Kwa hakika naona ni mahali pa wahusika kama Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kueleza jicho.**

TARURA iko nchi nzima. Hapo niseme, kulikoni halmashauri zingine zinafanya vizuri. Mkikaguliwa, naamini baadhi ya maeneo mna maandiko bora kujieleza, lakini haifanani na kilichoko penye ushuhuda. Kwa hakika naona ni mahali pa wahusika kama Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kueleza jicho.

Hapa kwetu mkoani Mwanza, nikitupa jicho wilayani Magu kuna ushuhuda ninaona magumu ya barabara mbovu, mpaka madiwani wa halmashauri ya wilaya hiyo wanadiriki kuujia juu uongozi wa wasimamizi wa barabara mahali hapo.

Kipindi cha mvua, hata gari la kiongozi mwenyewe linaweza lisipite, lakini 'yote kwa yote' jibu linaangukia fedha zinazotolewa na serikali hazitoshelezi kugharamia miradi. Kwa hiyo wananchi tuanze kubeba majembe, sululu na mabeleshi, kwenda kutengeneza barabara hizo kwa nguvu zetu badala ya kutumia makandarasi wenye vifaa kama katapira na guludozo la kushindilia udongo barabarani ili kuwa imara yenye ubora.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali ya Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, hivi hakuna njia nyingine ya kusimamia TARURA na kuwabana wahusika wa kulea magumu ya miradi yetu wananchi mpaka, naomba tubebe.

Sasa Waziri Ummy nina maoni kwamba, huu ni wakati wa kukunjua makucha na kuwafinya wanaokujaribu kila mahali TARURA iliko, ili waache kufanya kazi kwa mazoea kama walivyozoea na kutengeneza taarifa za mezani (kama zipo) kukuridhisha, hasa unapokwenda ziara za kikazi.

Watanzania wenzangu hivi kila kitu ni kuchakachua tu, hatuna kizuri? Maana hata kizuri huharibiwa ladha yake na kuwa chachu, kama ni chakula ukiletewa wali unachanganya tena na mchanga, kama ni mfuko wa sukari kilo 50 unatobolewa tundu zinabaki kilo 49, halafu muuzaji anakwambia ni ujazo uleule.

## Matokeo chanya ya TASAF sekta elimu

**Na Elizabeth Zaya**

MPANGO wa Kunusuru Kaya Maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wilayani Mkuranga mkoani Pwani umeanza kuzaa matunda katika eneo la elimu baada ya wanafunzi waliopo kwenye kaya za walengwa kuanza kuhitimu vyuo vikuu huku wengine wakinufaika na elimu ya ufundi stadi.

Mratibu wa TASAF Mkuranga, Safina Msemo, alisema wanafunzi sita walioko kwenye kaya za walengwa wamefikia elimu ya juu na kwamba watatu ni wa kike na watatu wengine ni wa kiume.

Pia, alisema wapo vijana 32 kutoka katika kaya hizo za walengwa waliopata mafunzo ya ufundi umeme, magari, udereva, usindikaji wa vyakula pamoja na utengenezaji wa batiki kutoka katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Ikwiriri na Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO). Mbali na hayo, Msemo alisema wanafunzi wengine kwenye kaya hizo wanasoma kidato cha sita na maendeleo yao ni mazuri.

"Mpango huu umekuwa na manufaa kwa walengwa wengi walioingia kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini kwa Wilaya ya Mkuranga, miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango huo ni kuongezeka kwa watoto wanaohudhuria shuleni na kliniki baada ya kutimiziwa mahitaji muhimu ikiwamo sare za shule, daftari, mabegi, nguo za michezo pamoja na lishe bora," alisema Msemo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Mwantum Mgonja, alisema jumla ya kaya 1922 katika wilaya hiyo zimepitishwa kuingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya maskini.

Pia, alisema jumla ya vikundi 205 vya walengwa vya kuweka akiba na kuwekeza vimeundwa na kwamba kati ya hivyo 156 vimesajiliwa kwenye mfumo wa Benki Kuu.

Mgonja alisema kaya nyingi za walengwa katika wilaya hiyo kwa sasa zimemudu mahitaji ya msingi ikiwamo ya kuwa na chakula cha uhakika, mavazi na makazi ya kudumu.

"Baadhi ya kaya zimejenga nyumba bora, kukarabati, na kununua vifaa vya ujenzi kama mabati, saruji, na kuweka umeme wa jua. Wamebuni miradi midogo ya kujiongezea kipato kama vile ufugaji wa kuku, bata, mbuzi na mama lishe," alisema Mgonja.

"Walengwa wameanza kununua mbegu bora na dawa za kuua wadudu ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, haya ni maendeleo makubwa ambayo yamepatikana huku kwetu kupitia TASAF."

# RC apigia debe jitihada kunadi utalii

**Na Francis Godwin,** IRINGA

SERIKALI ya Mkoa wa Iringa imetaka jitihada zilizoanzishwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Brand Tanzania Initiative (BTI) kwa kutangaza fursa za utalii ndani ya mkoa, ziungwe mkono.

Jitihada hizo zimeelezwa kuwa zinashabiana na mkakati wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kutangaza utalii wa Tanzania duniani kupitia kampeni maarufu ijulikanayo kama The Royal Tour. Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, alitoa rai hiyo jana katika ukumbi wa Iringa Sunset wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa wafanyakazi wa BTI.

Alisema lengo la serikali ni kuona sekta ya utalii inatangazwa zaidi duniani na kupitia sekta hiyo serikali inakuza uchumi wake kwa watalii zaidi kuingia nchini.

Sendiga ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, alisema moja ya maeneo ambayo yanaweza kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea vivutio vya utalii ndani ya mkoa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya viwanja vya ndege.

Mkuu wa Mkoa alisema kazi hiyo kwa Iringa imeendelea kufanyika kwa Uwanja wa Ndege wa Iringa, maarufu kama Nduli, kuboreshwa na ifikapo Machi, mwakani, utaanza kutumika.

Pia alisema serikali ina mpango wa kuweka kituo cha utalii eneo la Kihesa Kilolo ambacho wakati wowote kitaanza kujengwa kwa kuwa mipango yote iko tayari.

Alisema iko miradi ya uendelezaji wa utalii mikoa ya kusini (REGROW) inayoendelea kazi ikiwa ni pamoja na kusogeza umeme katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kuboresha barabara ya kwenda kwenye hifadhi hiyo kwa kiwango cha lami.

Jitihada zinazofanywa na BTI, alisema zinakwenda sambamba na za Rais Samia kupitia filamu aliyoirekodi ya The Royal Tour, hivyo serikali ya mkoa haitakubali kuona kuna mtu anakwamisha jitihada za BTI katika kutekeleza majukumu yake ya kutangaza fursa za utalii ndani ya mkoa.

Katibu Mtendaji wa BTI, Lusekelo Mwandemange, alisema taasisi hiyo yenye miaka tisa sasa lengo lake kuu ni kuitangaza nchi kimkakati pamoja na kujenga ushindani wa nchi.

Alisema taasisi hiyo inaundwa na vijana kutoka nchi nzima na kuwa kazi yao kubwa ni kufanya uchambuzi kitaifa na kimataifa, kuisaidia nchi kusonga mbele kimaendeleo na kufanya tathmini ya mambo mbalimbali kwa kuhusisha wataalamu tofauti.



Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, akizungumza na wananchi wa jimbo hilo, kwenye mkutano wa hadhara kueleza mambo ambayo ameyafanya ndani ya mwaka mmoja wa ubunge wake, ikiwamo katika sekta ya afya, elimu, ujenzi miundombinu ya barabara, madaraja, makalavati, pamoja na kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wamiliki ardhi wasisitizwa kulipa kodi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMISHNA wa Ardhi, Nathaniel Nhonge, amewataka watu wote wanaomiliki ardhi kulipa kodi ya pango ndani ya wakati ili kuepuka faini na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Nhonge alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungmza na waandishi wa habari kuhusu ulipaji wa kodi ya pango la ardhi nchini.

Alisema kila mmiliki wa ardhi anao wajibu wa kulipa kodi ya pango la ardhi kwa mujibu wa sheria kwa maendeleo ya taifa.

"Wote wanaomiliki ardhi wanao wajibu wa kuhakikisha wanalipa kodi ya pango la ardhi ili kuondokana na kulipa kwa riba au kufikishwa mahakamni kutokana na kulimbikiza madeni" alisema Nhonge.

Pia alisema kwa wale ambao wanalipa kodi ya pango la ardhi kabla ya Desemba 31 hawatatozwa riba kama wale ambao wanavuka kipindi hicho.

"Kodi hii inaanza kulipwa katika mwaka wa fedha unapoanza hivyo kwa wale ambao wanalipa katika kipindi cha miezi sita hawatakumbana na riba ya asilimia moja ya kuchelewa kulipa na wale ambao watalipa baada ya Desemba 31 basi watalipa na faini ya riba ya asilimia moja," alisisitiza.

Alisema kupitia mkakati wa miaka 10 wa kupima ardhi yote, wamepanga kuongeza kasi ya upimaji kwa kutumia kampuni zote 197 za kupima na kupanga ili kila mtu kumiliki ardhi na kulipa kodi.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masami, alisema katika mwaka huu wa fedha wamepanga kukusanya Sh. bilioni 221.

Alisema mpaka sasa wameshakusanya zaidi ya Sh. bilioni 60 na asilimia ya wanaomiliki ardhi ambao wamelipa kodi ya pango la ardhi hadi sasa ni asilimia 50.

"Kipindi hiki cha mwisho wa mwaka ndio wakati watu wanalipa sana kodi hii ili kuepuka kulipa na riba hivi sasa tunakusanya hadi Sh. bilioni tatu kwa wiki.

Tulikuwa tunapokea wamiliki wa ardhi wanaolipa kodi 250 kwa wiki lakini sasa baada ya kusambaza hati za madai tunapokea watu 890 kwa wiki wanaolipa kodi ya pango la ardhi," alisema.

Kadhalika, alisema kwa jiji la Dodoma walikuwa wanakusanya kati Sh. milioni 60 hadi 70 kwa wiki lakini hivi sasa baada ya kusambaza hati za madai kwa wamiliki wanaodaiwa kodi ya pango, wanakusanya Sh. milioni 200 kwa wiki.

Hata hivyo, aliwasisitiza wamiliki wa ardhi kuhakikisha kuwa wanalipa ndani ya muda ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

# MIAKA 12 BILA RASHID MFAUME KAWAWA

## • 'Simba wa Vita'; alama uwajibikaji; nembo ya siasa kitaifa

**Na Waandishi Wetu**

INAWEZEKANA wakawapo baadhi ya watu ambao hawajui, kutokana na sababu mbalimbali. Lakini inabakia ukweli leo ni kumbukumbu ya kitaifa, miaka 12 ya kifo cha Waziri Mkuu wa Pili wa Serikali ya Tanganyika Rashid Mfaume Kawawa, aliyeletea uhuru nchini.

Wakati mwingine inawezekana watu wakajiuliza mbona Kawawa jina lake halisikiki sana kama ilivyo kwa viongozi wengine zamani? Jibu ni jepesi tu kwa waliomjua, alikuwa mtu wa vitendo na siyo maneno, ila alichotekeleza kilikuwa na vishindo.

Kawawa, maarufu 'Simba wa Vita, alitumikia taifa lake kwa nyadhifa mbalimbali ndani ya chama-TANU na CCM na serikalini, kabla na baada ya uhuru. Alifariki, siku kama ya leo, mwaka 2009.

Hata unapomzungumzia Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kwa upacha wa kazi, hata uswahiba hapana shaka Simba wa Vita anajitokeza kwa kila hali. Alikuwa katika safu ya watendaji kitaifa waliokuwa na mchango mkubwa, kuanzia kuusaka uhuru hadi awamu ya kuuboresha.

Leo hii kihistoria, Tanzania haiwezi kukamilika bila ya kutaja jina la Rashid Mfaume Kawawa, kwani ana mchango usiojificha, kwa kila awamu.

Kimsingi, sifa yake kuu alikuwa na hulka ya uchapa kazi zaidi, ila si mwingi wa maneno. Pia ana eneo lingine la upekee, panapofikiwa uamuzi wa utekelezaji kitaifa, hapo ndipo panaposhuhudiwa 'U-Simba wa Vita' maana aliifuatilia hatua kwa hatua, jambo ambalo kihistoria lilimkuna sana Baba wa Taifa.

Akiwa ametangulia mbele miaka 12 iliyopita, Kawawa ana ubunifu unaouacha kihistoria nchini, kwani alipokuwa kijana wa miaka 29 tu, ana mchango wenye msaada mkubwa katika harakati za uhuru kwa kuhamasisha kwa mafanikio yaliyotakiwa na TANU, yeye akiwa Katibu Mkuu wa lililokuwa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini.

Hapo kuna mgomo mzito wa kampuni ya bia nchini na ule wa wafanyakazi wa Shirika la Reli, chini ya kofia ya Jemedari Christopher Kasanga Tumbo, hata kuliainisha nyendo za siasa za uhuru.

Hilo lilimkuna sana Mwalimu Nyerere, wakati huo akihangaika na TANU na hakusita kuomba faragha naye mwaka 1955 katika Mtaa wa Lumumba, Dar es Salaam, naye hakumkatalia hata chembe kwani 'angejua'?... tangu zama hizo akiwa mwanafunzi Tabora, alishakunwa mno na yale ya Mwalimu Nyerere, sambamba na mbia wake shuleni, Mwalimu (Balozi) Tibandebage.

Ni uswahiba uliodumu nyumbani na kazini kwa wasifu wa 'kufa na kuzikana', hata baada ya kufanikisha lengo lao la uhuru wa Tanganyika, Mwalimu Nyerere alimwamini kuliko maelezo, akidiriki kumkaimisha cheo cha ukuuu wa nchi - Waziri Mkuu.

Ni wakati huo Nyerere alihamia TANU kuiimarisha na aliporudi muda mfupi kabla ya nchi kuwa Jamhuri, 1962, ukuu wa nchi ukihamia urais, daima kila kitu kilipita kuwa sawa chini ya Kawawa.

Aliporejea kwenye kiti cha usaidizi, hakupumzika akiendeleza rekodi ya uchapakazi na ubunifu, mfano hai alibuni kuanzishwa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) akashiriki akitumia hoja kwa vitendo, kuanzia 'ukuruta' hadi kumaliza, jambo ambalo vijana wa Kitanzania walipitia na wanaendelea kupitia.



Rashid Kawawa, wa pili kutoka kushoto mstari wa mbele aliposhiriki mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Kuna kinachozungumziwa sana hadi sasa, hasa safu ya uongozi ukinyooshewa kidole, suala la uadilifu, daima Kawawa anaacha rekodi, hata ikikumbukwa Nipashe ilipomtembelea nyumbani kwake Madale Dar es Salaam na kudai maoni yake, si kwamba aliishia kukiri dhana hiyo, aliiwekea msisitizo kuwa imani kwa viongozi.

Simba wa Vita alitoa mfano wa kwamba, zama zilizopita katika mikutano yao ya ndani ya kisiasa, walibishana sana kimsimamo, lakini walipofikiana wote walitii na kuufanyia kazi kwa juhudi na maarifa, tena umma haukupata nafasi kujua kilichojiri mkutanoni, zaidi ya ajenda zilizoafikiwa.

Haikushangaza uchapakazi wake kwa staili ya vitendo kuliko maelezo na historia ya alikotoka na kufanyia kazi TANU na CCM, pale chama kurejesha cheo cha Katibu Mkuu, Kawawa alikabidhiwa kiti kwenda kuweka sawa kwa vitendo kila kilichoamuliwa na chombo hicho, pia Mwenyekiti Nyerere, aliyekuwa na jukumu lingine la kuongoza serikali.

Kawawa alistaafu akiwajibikia CCM chombo alichoanza kukitumikia katika ujana, akishika usukani kuwapigania wafanyakazi, kwa historia inayoshabihiana kwa karibu na Chama cha Labour, nchini Uingereza.

**UTASHI WAKE**

Mwandishi wa makala hii alishuhudia namna utashi na uzalendo kwa mambo makuu mawili ya mfano, mosi katika mazungumzo ya Madale, Kawawa akiwa yu dhaifu mgonjwa, ghafla alipogusiwa kuhusu matembezi ya hiari kama yalivyo ya Azimio la Arusha, alionyesha tabasamu na hamasa kubwa hata kuanza kutoa darasa inavyofanikishwa.

Haikuishia hapo tu, katika hali hiyo, aliamua kuwasindikiza wageni wake (mwandishi na mpigapicha) hadi penye gari lao na kuwapungia mkono kwa tabasamu na bashasha. Hiyo ilikuwa miaka nane kabla ya kifo chake.

Tukio la pili, ilikuwa mwaka 2006 katika Uwanja wa Ndege Mdogo wa Misheni ya Mbesa, Tunduru mkoani Ruvuma kuzindua kampeni za CCM za uchaguzi mdogo wa ubunge.

Baada ya kutua na ndege ndogo, alipoingia ukumbini akaanza kuimbiwa wimbo mkongwe alioufanyia kazi sana wa "Eeeh TANU Yajenga Nchi..." waimbaji wakiwa wazee wenzake, ulimkumbusha mbali kihisia kama zile za matembezi ya hiari.

Lakini, safari hii alishindwa hata kutamka neno zaidi ya kutokwa na machozi kwa wingi, hata waimbaji wakalazimika kuukatisha wimbo na kumpa muda wa kutosha kujipanga, kabla ya kuanza kuzungumza.

**VITENDO KULIKO KAULI**

Katika dhana 'Hapa Kazi tu!' hapana shaka Kawawa ni mwenyeji. Hulka yake hakuogopa kutekeleza magumu yenye manufaa kwa taifa, kwani hata baada ya nchi kupata uhuru, hasa baada ya 1964, mwaka wenye mengi mazito kuamuliwa, kuna mengi yenye mkono wake kushuhudiwa

Mwalimu Nyerere na vyombo vyake, walipoamua na kuelekeza macho na hisia, uamshaji miguu, mikono, viungo vingine na nyenzo za kufanya kazi, ama moja kwa moja au nyuma ya pazia, ilikuwa kazi ya Simba wa Vita.

Mfano hai wa kurejea ni kilichoamuliwa kupitia Azimio la Arusha, 1967 na mengi yaliyoendana nalo hadi miaka ya 1970 yote, kiranja mkuu wa mbunifu na mfuatiliaji ni 'Simba wa Vita'. Hapo hapawezi kusahauliwa ujenzi wa nyumba za mikopo ya wananchi nchi nzima mwaka 1966, chini ya Shi.

Penye uanzishwaji wa Vijiji vya Ujamaa 'Operesheni Vijiji' 1974; kuanzisha maduka ya ushirika, Operesheni Ngua Fupi; Operesheni Njaa, Kazi ya Kawawa ilionekana kwa uhakika.

Kimsingi, alisimamia maeneo mengi kikamilifu bila ya woga wala kusita, hadi akapapichwa jina hilo la 'Simba wa Vita' na hata katika utafsiri iko wazi na sifa ya kuta 'Pacha wa Kazi wa Nyerere'.

Kawawa alikuwa mpole, lakini mkali kwa wasiotekeleza wajibu wao kikamilifu. Hakusita kuchukua, kutekeleza uamuzi mgumu. Leo hii anapokumbukwa, Rashid Mfaume Kawawa, anabaki nembo na ishara ya siasa.

**Makala hii imeandaliwa na Peter Orwa na Sabato Kasika**



Rais Julius Nyerere, alipokuwa na Rashid Kawawa. **PICHA ZOTE: MAKTABA .**

## NAIC yatakiwa kuhimilisha ng'ombe milioni moja kwa mwaka

**Na Mbaraka Kambona**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amekitaka Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kilichoko mkoani Arusha kufikia lengo la kuhimilisha ng'ombe milioni moja kila mwaka ili ifikapo 2025 wafikie lengo la kuhimilisha ng'ombe milioni tano.

Waziri Ndaki alitoa maelekezo hayo Desemba 29, 2021 wakati akikabidhi basi jipya kwa kituo hicho ili waweze kulitumia katika shughuli zao za kila siku za mafunzo kwa vitendo na kuwapeleka wataalamu katika kambi za uhimilishaji.

"Niwatake NAIC na wataalamu waliofundishwa kuhimilisha wahakikishe tunahimilisha ng'ombe milioni moja kama lengo letu linavyotutaka kwa mwaka huu na usafiri huu tunaoukabidhi leo utusaidie kufikia lengo hilo," alisema Ndaki.

Aliwataka NAIC kutunza vitendea kazi wanavyopatiwa na serikali ili viweze kuwasaidia kufanya kazi yao kwa ufanisi na kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

Vile vile, alisema wanataka kuona kituo cha NAIC kinarudi katika hali yake ya mwanzo ya kufanya kazi kama ilivyokusudiwa ya kutoa utaalamu wa uhimilishaji wa mifugo nchini.

Awali, Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Bedan Masuruli, alisema wizara ilitenga Sh. milioni 100 kwa ajili ya kununua basi hilo ambalo wanatarajia litasaidia kituo cha NAIC kufanya shughuli zake za mafunzo kwa vitendo na kuwapeleka kwa wakati wataalamu katika kambi za uhimilishaji.

Naye Kaimu Mkurugenzi, NAIC, Dk. Dafay Bura, aliishukuru serikali kwa kuwapatia basi hilo ambalo litawasaidia kutatua kero yao ya muda mrefu ya usafiri na kuahidi watalitunza na kulitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

# Uchimbaji madini salama ajenda ya kudumu - Biteko

**Na Mwandishi Wetu**

WACHIMBAJI wa madini wametakiwa kuzingatia uchimbaji salama katika maeneo ya migodi yao ili waweze kufanya shughuli za uchimbaji madini kwa tija na migodi iendelee kubaki salama.

Hayo yameelezwa na Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, juzi alipokutana na wachimbaji wa madini ya dhahabu katika eneo la machimbo la Nyamalimbe Makarashani lililoko Wilaya ya Geita, mkoani Geita.

Dk. Biteko aliwaagiza pia wakaguzi wa mgodi katika machimbo hayo kuweka utaratibu wa daftari kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu kwa kusainisha majina ya wachimbaji wanaoingia na kutoka katika machimbo hayo.

"Wasimamizi wote mnaosimamia hapa, hakikisheni watu wanaoingia kwenye duara kabla hajaingia kuna daftari juu limeandikwa anatoka wapi na umri wake, anapozama na kutoka anasaini tena," alisema.

Kuhusu umuhimu wa kulipa kodi, Dk. Biteko alisisitiza kila gramu ya dhahabu inayopatikana ipelekwe kwenye masoko ya madini ili serikali ikusanye kodi.

Pia amemwagiza Ofisa Madini Mkazi wa Geita, Daniel Mapunda, kutafuta wanunuzi wa madini ya dhahabu (Brokers) ili wasaidie kupunguza changamoto za wachimbaji kwenda umbali mrefu hadi Katoro kwa ajili ya kwenda kuuza dhahabu zao.

Kuhusu changamoto walizonazo hususani ya nishati ya umeme katika eneo hilo la machimbo, aliwahakikishia suala hilo limefanyiwa kazi kwa ushirikiano na Wizara ya Nishati ambao watafika kwa ajili ya kuwapatia umeme.

Aidha, aliagiza mialo yote iliyopo katika maeneo ya maduara ya shughuli za uchimbaji madini yaondolewe ili zihamishiwe kwenye maeneo rasmi yaliyotengwa kwa ajili ya kuweka mialo hiyo.

Akizungumzia kuhusu kulinda afya za wachimbaji, alisisitiza wachimbaji wa Nyamalimbe kulinda afya zao kutokana na maradhi mbalimbali.

Alisema, sehemu zenye shughuli za uchimbaji wa madini zina neema, lakini zina changamoto endapo mchimbaji hatazingatia taratibu za afya.

Naye Jumanne Amani akisoma risala kwa niaba ya wachimbaji wa Nyamalinde alisema, uwapo wa mgodi katika eneo hilo umeboresha maisha ya wakazi katika maeneo yanayozunguka mgodi huo na maeneo mengine ya watu wanaofika kujipatia kipato pamoja na kuboresha miundombinu ya barabara.

Alisema wachimbaji wanaomba kupatiwa huduma ya umeme katika eneo la mgodi ili kupunguza gharama za uendeshaji kwa wachimbaji na kuongeza tija.



Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, akizungumza na wachimbaji wa madini ya dhahabu katika eneo la machimbo la Nyamalimbe Makarashani Wilaya ya Geita mkoani Geita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hospitali magonjwa ya mlipuko yaanza kujengwa Shy

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

HOSPITALI ya magonjwa ya mlipuko ukiwamo wa COVID-19 imeanza kujengwa mkoani Shinyanga ili kuanza kutoa huduma ya matibabu kwa magonjwa hayo.

Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, alisema juzi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika jimboni kwake ndani ya mwaka mmoja wa ubunge wake, pamoja na kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Katambi ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, alisema katika kuendelea kuboresha huduma za afya jimboni kwake, wameshapata Shilingi bilioni moja, kwa ajili ya kujenga hospitali ya magonjwa ya mlipuko ukiwamo wa COVID-19, kwa sasa ujenzi huo upo hatua ya msingi.

"Ndani ya mwaka mmoja wa ubunge wangu katika Jimbo hili la Shinyanga nimefanya maendeleo makubwa, ikiwamo kuboresha huduma za afya na sasa tumeanza kujenga hospitali ya magonjwa ya mlipuko, wagonjwa wa COVID-19 watakuwa wakitibiwa hapa Shinyanga," alisema Katambi.

"Ikishakamilika hospitali hii ambayo kwa sasa ipo hatua ya msingi, wananchi kutoka maeneo mbalimbali watakuwa wakija kupata huduma hapa Shinyanga na kutakuwa na mwingiliano wa watu wengi sababu itakuwa (Medical Tourism), tutaongeza mapato na mzunguko wa fedha," aliongeza.

Alitaja mafanikio mengine aliyoyafanya ndani ya mwaka huo mmoja kwa upande wa sekta ya elimu kuwa alitoa Sh. milioni 34.2 fedha za mfuko wa jimbo, kwa ajili ya kuunga mkono ujenzi wa madarasa ambayo yalianzishwa kwa nguvu za wananchi.

Kwa upande wa miundombinu ya barabara, alisema zimeboreshwa katika maeneo mengi ya Manispaa ya Shinyanga yakiwamo korofi na kujenga madaraja na makaravati.

Akizungumzia masuala ya ardhi, alisema tayari wameshapata Shilingi bilioni moja, kwa ajili ya kupima, urathimishaji na uthamini wa maeneo, ili wananchi wapate hatimiliki na kwenda kuzitumia katika mambo mbalimbali ya kiuchumi.

Katika hatua nyingine, alisema mwaka fedha ujao (2022-2023) amejipanga kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ukiwamo ujenzi wa stendi kuu ya mabasi, soko, maegesho ya malori na ujenzi wa chuo kikuu, miradi hiyo itaanza kutekelezwa katika mwaka huo wa fedha.

Pia aliahidi kuendelea kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wa jimbo hilo, likiwamo suala la umeme, maji, miundombinu ya barabara, madaraja na makalavati, katika maeneo ambayo bado yana ukosefu wa huduma hizo.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, pamoja na Meya wa manispaa hiyo, Elias Masumbuko, kwa nyakati tofauti wakizungumza kwenye mkutano huo, wameahidi kuendelea kushirikiana na Mbunge Katambi, kufanya kazi ya kuwaletea maendeleo wananchi.

# JWTZ kusherehekea Mwaka Mpya kivingine

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Ulinzi wa Wananchi Tanzania (JWTZ), limetoa msaada wa vyakula na vitu mbalimbali kwenye vituo vitatu vya watoto wenye uhitaji, kwa ajili ya kuonyesha upendo kwa kuwawezesha kusherehekea vizuri sikukuu ya mwaka mpya.

Kamanda wa Kikosi namba 511 kilichoko Gongo la Mboto jijini Dar es Salaam, Kanali Amani Siyani, alivitaja vituo hivyo kuwa ni Uhai Development Organization, Kind Africa vilivyoko Chanika na Tankids Coming Home.

Zawadi zilizotolewa zina thamani ya Sh. milioni 7.5 kwa kila kituo kupewa vitu vyenye thamani ya Sh. milioni 2.5 huku vitu vilivyotolewa ni mchele, unga, mafuta ya kupikia na kupaka, sukari, maharage, sabuni, miswaki, dawa za meno, kalamu, madaftari na mashuka.

Kanali Siyani alisema kila mwisho wa mwaka wanakusanyika pamoja na kufurahia kusherehekea, lakini wakati huu wameamua kusherehekea kwa namna tofauti kwa kuwawezesha watoto wasiojiweza ambao sehemu ya jamii wanayoilinda. "Kwa kawaida kila inapofika Mwaka Mpya tunakaa na familia zetu au jamii zetu tunakula, tunakunywa na kufurahi. Lakini tunasahau kwamba kuna watoto maelfu wameachwa bila msaada. Tumeona tuwakumbuke hawa wenye uhitaji ili kwa pamoja tusherehekee Mwaka Mpya," alisema na kuongeza;

"Badala ya kukaa tukafurahia wenyewe na familia zetu tukaamua tuwasaidie wasiojiweza tuwapatie kile chote tulichokichanga kwa ajili ya kusherehekea ili na wao wakafurahie mwaka mpya, na kwamba lengo ni kujenga taswira nzuri kwa jeshi."

Alisema kufanya hivyo ni chachu kwa wengine huku akiwataka Watanzania kujitoa kwa ajili ya watoto wenye mahitaji ambao ni taifa la kesho na kwamba kwa kufanya hivyo watabarikiwa.

"Sisi wanajeshi kama sehemu ya jamii tunaona na tunatambua ugumu wa jukumu hili la kuwatunza watoto wenye uhitaji changamoto za kuwatunza hawa vijana ziko nyingi hivyo leo 'jana' tutajaliwa kutatua miongoni mwa changamoto zinazowakabili," alisema Kanali Siyani.

Msimamizi wa kituo cha Uhai Development, Teddy Kachwande, aliwashukuru wanajeshi hao kwa msaada ambao waliwapatia akisema utawasaidia kuwafanya watoto hao wafurahie sherehe ya mwaka mpya pamoja na siku zingine. Pia alibainisha kero zinazowakabili katika kituo hicho ikiwamo upungufu wa sehemu ya malazi, magodoro na vitanda, akidai kuwa wanawasimamia watoto 31 na miongoni mwao ni yatima, wanaoishi katika mazingira magumu na wale ambao wazazi wao wapo lakini wahana uwezo wa kuwalea.

"Changamoto (kero) nyingine ni huduma ya matibabu ambapo kati ya watoto 31 wenye bima ya afya ni sita tu, changamoto ya usafiri tukipata mgonjwa hadi tuanze kutafuta nani tushirikiane nae kwani hatuna mfadhili yeyote anayetusaidia.

"Mbali na changamoto hizo, tunaendesha shughuli mbalimbali katika kituo chetu kama ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi, kuku, kilimo na bustani, ambazo zinatusaidia kwa chakula na mahitaji mengine wa kuwatunza watoto, hivyo tunaomba kwa yoyote atakaeguswa aweze kutusaidia," alisema Kachwande.

Katika hatua hiyo, makamanda wawili wa JWTZ ambao hawakutaka majina yao yaandikwe, mmoja aliahidi kuwakatia bima ya afya watoto wanne na mwingine kumsomesha mtoto mmoja kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Mmoja wa watoto wa kituo cha Kind Africa, Sabia Fabihani, aliwashukuru wanajeshi kwa msaada huo na kutoa wito kwa Watanzania wengine kuiga mfano huo.

Naye Rajabu Salum ambaye analelewa katika kituo cha Tankids, alisema jambo walilolifanya wanajeshi hao ni la kipekee na kwamba uwe mfano kwa watu wengine kujitoa na kwamba kuna watu wengi wanahitaji misaada.



Meneja Mkuu wa Mgodi wa Dhahabu wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko (watatu kushoto), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari waliotembelea sehemu ya mradi wa mitambo mipya ya kusafisha maji, baada ya kutangaza kufikia lengo la uhifadhi wa mabaki ya taka zitokanazo na mchakato wa uchenjuaji wa madini, mgodini hapo wilayani Tarime, juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Wanafunzi 24 Kahama wapata ujauzito Jan-Oktoba

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

JUMLA ya wanafunzi 24 kutoka katika shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga wamepata ujauzito wakiwa masomoni kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari, hadi kufikia Oktoba 2021.

Kundi la wanafunzi waliooeshwa katika kipindi hicho walikuwa wawili na wengine wakifikishwa katika vyombo vya sheria na kesi zao bado zinaendelea.

Hayo yalisemwa juzi na Mkaguzi wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto, Tiho Masatu, katika mahojiano na gazeti hili kuhusu hali halisi na changamoto zilizoikumba dawati la jinsia katika kituo cha Polisi Kahama.

Masatu alisema kundi kubwa ambalo linaharibu wanafunzi kwa sasa kwa kiwango kikubwa ni madereva bodaboda huku akiwataka wazazi kuacha tabia ya kuwachanganya watoto wao na wageni wakati wa kulala chumba kimoja.

Alisema kuna baadhi ya watuhumiwa waliokwisha kamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria ikiwa ni pamoja na mahakamani na kesi zao bado zinaendelea kusikilizwa na mamlaka hiyo.

Alisema vitendo hivyo vinavyofanywa na makundi hayo kwa wanafunzi ni ukatili wa kijinsia kwa kuwa wanawapotezea wanafunzi kukamilisha ndoto zao za maisha na mtoto kukosa elimu ni moja ya ukatili wa kijinsia.

Alisema Dawati la Jinsia wanajihusisha na masuala ya kubaka pamoja na mimba kwa wanafunzi ikiwa ni kuibua matukio ya ukatili wa kijinsi ndani ya jamii iliyopo ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya mabadiliko.

Alisema katika kipindi hiki wanafunzi wengi wakipata mimba jukumu wanaachiwa wazazi kutokana na wanaume waliowapa ujauzito kutojitambua.

Alisema wazazi wengi hawawafuatilii watoto wao katika mienendo yao ya kila siku na kuongeza kuwa ni bora mwanafunzi anapokuwa shuleni kuliko akiwa nyumbani wakati wa likizo kwa kuwa mazingira ni hatarishi.

"Kutokana na changamoto hizo katika familia ambazo wanafunzi wamekuwa wakitoka tunaamini kuwa ni bora mwanafunzi anapokuwa shuleni anakuwa salama zaidi kuliko nyumbani kwani familia zimekuwa zikielekeza mambo mengi katika shughuli za kimaisha kuliko kumwangalia mtoto," alisema Masatu.

Alisema wazazi wengi wameshindwa kutatua changamoto nyingi katika familia zao kutokana na hali hiyo dawati hilo la jinsia lipo kwa ajili ya wanawake pamoja na wanaume.

Aliwataka wazazi kuacha tabia ya kuondoka asubuhi na kurudi nyakati za usiku huku wengine wakiwa wamelewa bila ya kuangalia watoto wanaendeleaje.

Alisema mimba nyingi zinatoka kwa watu ambao wanawafahamu kwa ukaribu uliopo baina ya famila na mtu husika.

# 'Wazee wasio na wake waongoza kwa ubakaji'

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WAZEE wasio na wenza wao (wake) majumbani wamedaiwa kuwa chanzo cha kujihusisha na matukio mengi ya ubakaji wa watoto katika jamii.

Imeripotiwa kuwa kesi nyingi za ubakaji zilizoko katika mahakama nyingi nchini zinahusisha makundi ya wazee jambo linalopaswa kukemewa.

Mkaguzi wa Jeshi la Polisi na Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Wilaya ya Kahama, Tiho Masatu, alisema hayo alipokuwa akiongea na mwandishi wa habari hizi kuhusu changamoto mbalimbali zinazolikabili dawati hilo.

Masatu alisema, kutokana na wazee kutokuwa na wake katika familia zao wanakimbilia kwa watoto, hali ambayo ni kinyume cha maadili ya kitanzania na kosa kubwa katika jamii na taifa.

Alisema kuwa wazee wengi wakati wa ujana wao hawakuweza kujali familia zao hali iliyosababisha nyumba zao kuvunjika mapema na kukosa wenza na kuamua kumaliza haja zao kwa watoto.

"Kuna mzee mmoja alihukumiwa hivi karibuni kifungo cha maisha jela katika Mahakama ya Wilaya ya Kahama kutokana na kosa la kumbaka mtoto mdogo tena wa miaka miwili, hali hii ni hatari sana kwa makundi hayo na elimu inatakiwa kutolewa ili kukomesha tabia hizo," alisema Masatu.

Akizungumzia chagamoto zinazolikabili dawati hilo la kijinsia katika Kituo cha Polisi Kahama, Mkaguzi huyo alisema wazazi wengi wanashiriki kuharibu kesi zinazowakabili watoto wao za ukatili wa kijinsia.

Alisema wazazi wanaahidiwa zawadi zisizotekelezeka na watuhumiwa hali inayowasababishia waathirika kupata tabu kutokana na washtakiwa kutokomea kusiko julikana.


Masatu alisema changamoto nyingine ni kundi la kinababa kuona kuwa wana haki ya kupiga wake zao kisheria jambo linalowaathiri wanawake.

Alisema kuwa katika familia nyingi kinamama hawana sauti ya kuongea au kurudisha maneno baba anapokuwa akiongea na akifanya hivyo anakumbana na kipigo ambacho mara nyingine kumsababishia mke kupata kilema cha maisha.

Alisema suala la mila na desturi hasa kwa makabila yaliyopo katika maeneo hayo pia ni moja ya changamoto kubwa inayomfanya mwanamke kuwa chini ya mwanamume siku zote na jamii inapaswa kupewa elimu kubwa.

Alisema dawati hilo wilayani hapo linatoa elimu mbalimbali kwa kushirikiana na vyombo vya habari hasa katika maeneo ya shuleni na kata mbalimbali kwa lengo la kuibadilisha jamii.

Ukurasa 13




Hebu tukae chini na tutafakari majina haya!




**MUHOGO SASA UNALIPA...**
**TOSCI yawavusha wakulima, wadau wake kutoka 'mbegu zembe' hadi mpya kisasa**

Ukurasa 12



# Mwekezaji mzawa Lake Oil ajitosa kuhudumia mafuta viwanja ndege

- Dhamira ya 2018 inaanzia KIA, Iringa, Dar
- Meneja: Tumeajiri 6000, akiba ipo lita mil 18

**Na Julieth Mkireri**

RAI na kilio kikubwa katika uongozi kitaifa, kwa awamu mbalimbali inayojumuisha ya sasa, dhima ni kuongeza uwekezaji kwa kiasi kikubwa, safari kuelekea Tanzania ya Viwanda, ambayo nchi sasa imeshakanyanga.

Ni tafsiri ambayo ndani yake kuna dhana ya uwekezaji kiuchumi, ambayo inafungua mengi katika safari ya maendeleo kitaifa, kuongeza pato la kodi kitaifa, ajira kwa umma, na mzunguko wa fedha wenye sura ya kukuza uchumi.

Hapo kuna suala la kuongezeka pato la mtu mmoja mmoja, vitengo vinabadilishana maisha hadi kufikia ngazi ya kaya.

Ndani ya suala la kuhamasisha uwekezaji wa ndani ya nchi, wenye tafsiri inayojumuisha kuweka msukumo wa maendeleo katika sura ya kimataifa, pia wakati.

Uhamasishaji wa kaulimbiu ya Tanzania ya Viwanda, umeenda sambamba na kuboresha mazingira ya uwekezaji, ikiwamo kuondoa vikwazo vilivyokuwa vikielezwa awali katika taasisi wezeshi.

Kuna sekta ya gesi na mafuta ambako bidhaa petroli inatumika kwa wingi nchini, kwa matumizi ya nyenzo za usafiri kitaifa na kimataifa, ndege, treni, magari. Vivyo hivyo ni katika matumizi ya nyenzo kama jenereta.

Mafuta ni nyenzo muhimu, ambayo biashara yake inaendeshwa na kampuni nyingi, kuanzia zinazomiliki huduma za usafiri kama treni, lakini wengi ni wamiliki binafsi wanaowauzia wahitaji .

Hapo ndiko inakopatikana kampuni ya Lake Oil, yenye zaidi ya miaka 10 iliyopita, ikijishughulisha na usambazaji mafuta, ndani na nje ya Tanzania, ikijenga vituo vyake vya mafuta ndani ya Afrika Mashariki.

Meneja Mshauri wa Kitengo cha Anga, Ismail Elagib, anaiambia Nipashe kuwa, mbali na uamuzi wa kusogeza huduma karibu waliko wateja, mjini na vijijini, pia imeanza kutoa huduma ya mafuta ya ndege kwenye usafiri wa anga

Ismail anafafanua kwamba, kampuni hiyo imeshapatiwa kibali cha kuanza kutoa huduma katika viwanja vitatu vya ndege nchini, ambavyo ni Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA), Kiwanja cha Ndege cha Iringa na Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Meneja huyo anaeleza kwamba katika mikakati ya kuongeza uwekezaji nchini, walipata wazo la kuanza kuhudumia kwenye usafiri wa anga tangu mwaka 2018 na mwezi uliopita - Novemba, ndio walianza kutoa huduma hiyo baada ya kukamilisha uwekezaji KIA, akifafanua kwa sasa wamekamilisha ujenzi wa miundombinu katika kiwanja hicho cha ndege.



Meneja Mshauri wa Kitengo cha Anga wa Lake Oil, Ismail Elagib. **PICHA: JULIETH MKIRERI.**

Pia, anafafanua kwamba Novemba 25, mwezi mmoja uliopita walishaanza kutoa huduma katika viwanja vya Iringa. Anasema katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, wanatarajia kuanza kuhudumia mwaka ujao 2022, unaoanza kesho, baada ya kukamilisha taratibu stahiki.

Anataja malengo yao katika miaka mitano ijayo wanakoelekea, ni kufikisha huduma bora katika viwanja vinginevyo, akifafanua wana maono yao, kufika Tanzania Visiwani na nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Ismail anaeleza kwamba, uwekezaji huo katika kusambaza mafuta ya ndege kwenye huduma za anga, unazingatia mwongozo wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Shirikisho la Mamlaka za Anga Duniani (IATA) na Muunganiko wa Kimataifa wa Usimamizi wa Mambo ya Mafuta ya Ndege (JIG).

Ismail anaeleza kwa sasa, kampuni hiyo ina jumla ya wafanyakazi 6,000 na kati yao wa kitengo cha anga wapo 16, wakijumuisha wabobezi kwenye tasnia ya mitambo na opareshéni ya mafuta ya ndege nchini, wanaotegemea kuongezeka baadae, kulingana na huduma zitakavyokuwa zikiongezeka.

"Lengo letu ni kutoa huduma bora na nafuu. Mipango mikakati yetu ni kufikia viwanja vya ndege katika mikoa yote hapa nchini na baadae nchi jirani," anaeleza.

Meneja huyo anafafanua kwamba, hadi sasa wataendelea kujifunza kwa kampuni nyinginezo zinazotoa huduma hiyo, pamoja na Muunganiko wa Kimataifa wa Usimamizi waMambo ya Mafuta ya Ndege (JIG), ili kusambaza huduma bora zenye kiwango cha kimataifa katika maeneo anakonuia kutoa huduma.

Ismail anasema, kwa sasa wana uwezo wa kutunza lita milioni moja katika kiwanja cha KIA na lita milioni 18 katika bohari ya kampuni iliyopo Kigamboni, Dar es Salaam, zinazoweza kuongezeka baadae, kulingana na ongezeko la mahitaji, kutegemea namna biashara itakavyopanuka.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Julius Ndyamukama, anafafanua kuwa Lake Oil ni kati ya kampuni wazawa zilizokidhi vigezo vya kutoa huduma ya mafuta ya ndege.

Ndyamukama anatoa wito kwa kampuni zinazotoa huduma kwenye mamlaka za anga, kuendelea kujiimarisha kwa viwango vyenye ubora na kupambana katika masoko ya ndani na nje ya nchi, kama ilivyo hatua ya wazawa Lake Oil.

BIASHARA

MUHOGO SASA UNALIPA...

# TOSCI yawavusha wakulima, wadau wake kutoka 'mbegu zembe' hadi mpya kisasa

- Soko la wazi, waliojaribu hawalijutii jembe lao
- Mkuranga 1, Chereko, Kipusa, Kiroba, Kikombe




Mkaguzi wa Mbegu kutoka TOSCI Makao Makuu Hemed Msofe (mwenye kofia) akimwelekeza mkulima Shabani Pilla (mwenye kaptula), namna ya kuendesha kilimo cha mbegu za muhogo kwa manufaa.

**Na Christina Haule, Chalinze**

ZAO la muhogo ni maarufu na hasa katika baadhi ya jamii nchini. Ni chakula cha manufaa ya ziada, katika tafsiri za kiuchumi na kiafya.

Kuna ukanda zao hilo linalimwa kwa kiasi kikubwa. Taasisi ya kudhibiti ubora wa mbegu Tanzania (TOSCI), nayo inaamua kuingilia kati, wanaaswa kutotumia mbegu za kienyeji, bali watumie zilizothibitishwa ubora na taasisi hiyo.

Ni aina ya mbegu anayoieleza inawaletea manufaa kwa mauzo ya mbegu na muhogo wenye masoko ndani na nchi za nje.

Mkaguzi wa Mbegu kutoka TOSCI Makao Makuu, Hemed Msofe, anasema alikokuwa Chalinze, mkoani Pwani, kwamba mkulima anayetumia mbegu za kienyeji kila mwaka, daima hatofanikiwa kupitia kilimo.

Kwa mujibu wa Msofe, baadhi ya wakulima huishia kubadilisha aina ya kilimo, kati ya mwaka mmoja na mwingine.

Anasema kulima kwa kutumia mbegu za kienyeji, kunatoa uwezekano mkubwa wa kusababisha mbegu au muhogo (mzizi) kupata magonjwa, ambayo mengine hayana dawa na kuleta madhara kwenye mfumo mzima wa uzalishaji zao hilo.

Mtaalamu huyo anafafanua kwamba, ushambuliaji mmea wa muhogo unajitokeza pale mkulima anakwama kufuata maelekezo ya matumizi ya mbegu bora, ambayo yanajumuisha 'michirizi ya kahawia' na 'batobato' ambayo husumbua mbegu na kupoteza ubora wake.

Anasema ni mwelekeo unaomsababishia mkulima kupata mavuno kidogo au yenye kiwango duni, hivyo uzalishaji unapungua. Pia, ni jambo linalojitokeza kwa mkulima mwingine anapotumia mbegu ya namna hiyo.

Msofe anataja magonjwa mengine, ni ya aina ya virusi vimavyoshambulia zaidi mzizi wa muhogo, ukinyausha mmea na kupoteza ubora wa mbegu husika.

"Matumizi ya mbegu za kienyeji zisizothibitishwa ubora na TOSCI, mara nyingi wakulima huwa hawana kanuni kwenye kilimo kwani hupata na kukosa mwaka hadi mwaka na mavuno huwa machache" anasema Msofe.

**NAMMA ZILIVYO**

Ofisa Kilimo wa TOSCI, Fredy Cyprian, anasema wameweka utaratibu wa kutenga wakala kwenye kila eneo zenye kanda za mbegu, ambako zinapatikana kirahisi kupitia mitandao ya jamii akifafanua: "Unabonyeza (kwenye simu) 'seed truck' na kupatikana wakala wote wa mbegu nchini."

Anasema, kupitia wakala hao kunapatikana mbegu aina mbalimbali, ambazo mkulima anashauriwa kuzitumia kulingana na ukanda wa kilimo aliyopo, akitoa mfano mkoani Pwani kunapatikana mbegu aina: Mkuranga 1, Chereko, Kipusa, Kiroba na Kikombe.

Anazitaja mbegu zingine za muhogo ni Momba na Mkumba, zinazolimwa katika kanda tofauti za kilimo nchini na kuwapa matunda wakulima.

Hata hivyo, anasema mbegu za muhogo hupandwa hadi kuvunwa kwa muda wa miezi 12 na mkulima anaweza akanufaika kwa hatua zaidi, TOSCI ikichukua jukumu hata kumtafutia soko mwekezaji.

**KINACHOFANYIKA CHALINZE**

Mkaguzi wa Mbegu aliyeidhinishwa na TOSCI kutoka Chalinze, Ahmed Mwarabu, anasema anaendelea kufuatilia na kusimamia kilimo cha mbegu za muhogo katika maeneo hayo, kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora zisizo na magonjwa, lengo ni kukuza uzalishaji na kuinua kipato cha wakulima.

Mmoja wa wakulima walionufaika na zao la muhogo Shabani Pilla, mkazi wa kijiji cha Kilemelemeta, Chalinze, anasema katika uwakala wa upatikanaji mbegu bora za kilimo cha muhogo, Kanda ya Chalinze, anakubali manufaa ya kilimo cha mbegu, akiwa analima shamba lenye ukubwa wa ekari mbili.

Pilla anafafanua, ni mradi unaotumia mtaji wastani wa Sh. 360,000 na baada ya mauzo ya mbegu anapata Sh. 2,160,000 jambo lililomuwezesha kujenga vyumba vitatu vya biashara kwa thamani ya Sh. milioni 1.5 anavyokusanya kodi na kumsaidia kutimiza majukumu yake ya kimaisha.

Anasema mapato mengine ya muhogo, anayatumia kusomesha watoto wake wawili walioko katika shule ya sekondari, huku kiasi kinachobaki anatumia kwa ajili ya kufanya palizi katika shamba lingine lenye ukubwa wa ekari mbili, ikiwa namna ya kuendeleza kilimo hicho cha muhogo.

Mkulima Pilla, anaiasa jamii ijikite kwenye kilimo cha muhogo, akiamini kwa ushahidi kwamba ina uwezo mkubwa wa kumuinua mkulima na kukuza uchumi wake, kwani kwa sasa kuna soko la bidhaa hiyo, ikiwamo muhogo wenyewe na mti wake, akimaanisha mbegu kwa matumizi ya wakulima wa zao hilo walioelimika kutoka kote nchini.

"Ukikosa mtego wa kuuza mbegu unatega kuuza mzizi ambao ndio mhogo, kwa sababu wapo wanunuzi wa mhogo, uwe mbichi au mkavu, ili mradi uwe umeuandaa wakiwemo raia wa China, hununua mhogo na kwenda kuutumia katika matumizi mbalimbali nchini mwao" anasema

Anaeleza kuwa shamba lenye ukubwa wa ekari mbili, mkulima anaweza kupata mavuno ya tani 15 hadi 30 za muhogo mbichi, lakini muhogo huo ukikauka unaweza kuwa na uzito wastani wa tani nane hadi 13 na kwamba mhogo mkavu unaweza kuuzwa kwa bei ya Sh.Milioni 1.5 hadi Sh. Milioni 1.7 kuna faida ya Sh. Milioni moja, baada ya kutoa gharama za zote za maandalizi ya kilimo.

Anaorodhesha gharama hizo kuwa ni kununua shamba kwa wastani wa Sh. 400,000 kwa ekari moja, kulima Sh. 60,000; na palizi mara mbili jumla ni Sh. 40,000.

**MKURUGENZI TOSCI**

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, anasema walisajili jumla ya mashamba ya zao la muhogo yenye ukubwa wa hekta 214 mwaka 2016 baada ya zao hilo kutengenezewa viwango stahiki (certification standards) zinazotumika katika upatikanaji mazao bora yanapopandwa.

Patrick anasema, hadi kufikia Oktoba mwaka jana, kuna mashamba yenye ukubwa wa hekta 426 ya mbegu bora za muhogo yalisajiliwa, sawa na ongezeko la asilimia 50.2 na kwamba katika msimu wa 2021/2022 wanategemea uzalishaji wa vipando vipatavyo 12,307,837 kutoka kwenye mashamba hayo.

Anafafanua vipando hivyo vinatarajiwa kupandwa kwenye jumla ya hekta 1230 sawa na ekari 3076, akiwaahidi wakulima watarajie upatikanaji mbegu bora za muhogo katika maeneo yote yanayostawisha zao hilo, ambako mwitikio wa matumizi ya mbegu za muhogo zilizothibishwa ubora yapo chini sana

Sababu ya kusuasua jamii kuelekea uzalishaji duni, unaanzia kutokuwapo uhamasishaji wa kutosha wa matumizi ya mbegu zilizothibitishwa ubora na kukosekana soko la uhakika la zao hilo.

Anaitaja kuwa chanzo kikuu kinachowafanya wakulima wasione tija ya kuingia gharama ya ununuzi wa mbegu bora, hata wakaendelea kutumia mbegu za misimu iliyopita.


TOSCI kwa kushirikiana na wadau wengine wa zao muhogo, iko katika juhudi za kufanya uzalishaji muhogo upate hamasa, pia kuhakikisha wakulima wa mbegu wanapatikana jirani na waliko wakulima, ili kurahisisha upatikanaji wa mbegu bora.



Mnufaika wa kilimo cha muhogo, Shabani Pilla, akiwa amesimama mbele ya jengo la biashara, katika kijiji cha Kimelemeta, Chalinze, baada ya mauzo ya muhogo. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Hebu tukae chini na tutafakari majina haya!






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

MIMI hupenda sana kusikiliza soka kupitia matangazo ya redio, ingawa pia napendelea kuangalia kupitia luninga na mara chache uwanjani.

Lakini, ninaposikiliza redio huwa napata mkanganyiko sana nisikiapo mtangazaji anasema tuko Uwanja wa Karume au Uwanja wa Jamhuri.'

Hukanganyikiwa hasa anaposahau kuniambia ni uwanja wa mkoa gani anaoutaja. Kwa sababu, najua viwanja vya Karume ambavyo ni kumbukumbu ya Rais wa Kwanza wa Zanzibar, marehemu Abeid Amaan Karume viko mjini Musoma, Mara na jijini Dar es Salaam.

Pia, najua viwanja vya Jamhuri viko Morogoro na Dodoma. Hapo sasa lazima namdai mtangazaji aniambie tuko Uwanja wa Karume Musoma au Uwanja wa Karume Dar es Salaam?

Pia, aniambie tuko Uwanja wa Jamhuri Morogoro au Uwanja wa Jamhuri Dodoma? Kinyume cha hapo, atakuwa hajanitendea haki na si mimi tu, bali na wasikilizaji wenzangu wengine wanaojua kuwapo viwanja hivyo vya kumbukumbu.

Huwa najiuliza mara nyingi, nini kigezo cha kutoa majina kwa maeneo kama hayo, ingawa najua ni kumbukumbu kwa heshima ya watu na au matukio yaliyopita, lakini yenye mchango mkubwa kwa taifa letu.

Hakuna asiyejua mchango wa Karume katika Taifa la Tanzania, akishiriki kikamilifu kuunganisha nchi za Zanzibar na Tanganyika Aprili 26, 1964 na kuzaa Tanzania. Hakuna asiyejua umuhimu wa nchi kuitwa Jamhuri na ndiyo sababu nchi inajitawala.

Pamoja na umuhimu huo, hivi lazima kila kitu kiitwe jina hilo hilo na iwe katika kila mkoa? Nadhani hapana. Ni kwamba, hata likiwa katika eneo au mkoa mmoja inatosha, kwa sababu ni suala tu la kumbukumbu, kwamba huyu alifanya hivi au kitu hiki kilitokea vile.

Naamini litafanyika jambo katika kuondoa mkanganyiko huu, ambao unanisumbua pengine si mimi tu bali na mamilioni ya wasikilizaji wenzangu. Karume Stadium ibaki moja, vivyo hivyo Jamhuri Stadium, hivi vingine viwili wapewe 'almaarufu' wengine.

Kama hilo litakubalika, basi vitumike vigezo ambavyo havitaleta shaka kwa watu.

Hakuna mtu anayeweza kupinga kuwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, katika stahiki yake kupewa kwa jina lake kuwa kumbukumbu ya mchango wake kwa taifa. Pia, zipo taasisi na shule mbalimbali hata mitaa na maeneo, zilizopewa majina ya watu.

Watu hao wengi wao ni waliotoa michango yao katika kulikomboa au kulijenga taifa hili kutoka minyororo ya ukoloni na ukandamizaji mwingine. Hawatoshi kutajwa mmoja mmoja katika safu hii, vinginevyo mtakuwa mnasoma daftari la majina hapa.

Kuna maeneo huenda kuna majina ya miundombinu inapewa katika maeneo fulani bila kuelezwa mchango wao uliotukuka.

Sina chuki na yeyote katika hao, ila ni busara kujifunza na kuijua yasirudiwe makosa ya ama kutoa majina au kuacha kutoa majina ya wananchi kimakosa.

Najua kabisa Patrick Mfugale, alikuwa Mhandisi mzuri wa madaraja na alifanya vizuri kama eneo lake la kazi, akapewa jina katika Daraja la Tazara.

Hali kadhalika John Kijazi, alifanya kazi ya uhandisi, pia Katibu Mkuu Kiongozi, akilipwa pia kwa kazi yake nzuri. Akapewa jina katika daraja kama la Tazara, pale Ubungo.

Katika vyote hivyo, aliyekuwa Rais Dk. John Magufuli alitolea ufafanuzi vigezo vya kina katika tukio hilo, akioanisha na wasifu wao kazini.

Spika wa Bunge Job Ndugai, ameifanya kazi yake kama mbunge na Spika bila kutetereka na alitarajiwa hivyo kwa mujibu wa majukumu na stahiki zake, licha ya changamoto za hapa na pale, kapewa jina la soko pale jijini Dodoma, katika pendekezo lililopitia mtiririko pacha kama tukio la Dar es Salaam.

Hapo ndipo ninapowakumbuka watangulizi wake, mathalan Chifu Adam Sapi Mkwawa, Pius Msekwa, Samwel Sitta na Anne Makinda, wana masoko au stendi au viwanja maeneo gani? Pengine nao wakumbukwe! Alamsiki!

BIASHARA

# Serikali yajitosa kuwekeza vituo vya petroli vijijini kuziba pengo

## • Vituo 100 vimeanza, vingine vyaja




Baadhi ya vituo vya mafuta katika miji midogo, jirani na vijijini. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MARA nyingi watu wanaosafiri umbali mrefu kwa mabasi au malori, iwe nchini au nje ya mipaka, wanashuhudia namna madereva wakibeba mafuta ya ziada katika matanki yao kwa ajili ya tahadhari.

Ni hali inayotokana na wasiwasi wa kuishiwa mafuta njiani, ambako huwa hakuna mahali ambapo hutoa huduma hiyo, hata wakikwama njiani.

Ukosefu wa visima vya mafuta katika maeneo ya pembezoni hasa vijijini, unatokana na uwekezaji mdogo ambao sekta ya umma na binafsi zinaufanya.

### TPDC YAAMUA

Katika hilo, Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini (TPDC) limeamua kujenga visima 100 katika maeneo ya vijijini, kupunguza tatizo hilo.

Je, ni kwa kiasi gani TPDC itafanikiwa ni swali linalohitaji muda kupata majibu. Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) nayo imekuwa ikichagiza watu mbalimbali kuwekeza katika maeneo ya vijijini, ambako kunajulikana kuko nyuma kimaendeleo, kulinganisha na mijini.

Hicho kinapafanya pawe na matatizo ya usafiri na usafirishaji, kwani magari machache yanafika huko, wakihofia kitendawili cha pa kupata mafuta ya kurudi.

Hata hivyo, kuna maendeleo yanayoendelea sasa vijijini, ambako kuna shule za msingi na sekondari, zahanati na vituo vya afya vilivyojengwa kwa vigae, marumaru, madirisha ya vioo na nondo.

Mfano mzuri ni kazi inayoendelea sasa ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kila shule kutokana na fedha, Sh. Trilioni 1.3 zilizotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), kama mkopo.

Ni wazi maendeleo ya sekta za afya na elimu vijijini hayawezi kutenganishwa na huduma za usafiri kutoka mjini, ambako vifaa kama saruji, nondo, madirisha ya vioo, marumaru, misumari vinapatikana viwandani na madukani.

Usafiri wa magari ndio unatumika kwa ulazima wa pekee.

Kwa muda mrefu, sekta ya mafuta nchini inayodhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imekuwa na changamoto ya mafuta hayo kuuzwa, kwa bei ghali kutegemea umbali yalikotoka. EWURA imekuwa ikiratibu bei za mafuta kila mwezi kulingana na mafuta hayo yanavyonunuliwa soko la dunia.

> **“Dk. Mataragio anasema vituo vitatu zaidi vitakarabatiwa mwaka huu wa fedha vya Makuyuni, Manyara, Singida na Geita. Anaendelea: “Tunataka kuwafikia wananchi wote na tumeona umuhimu wa kutoa huduma hii ya mafuta katika maeneo ambako haipo. “**

Meneja Mawasiliano kwa Umma Ewura, Titus Kaguo anasema, muda mrefu sasa wanapanga bei kwa kuzingatia umbali kutoka bandari za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara inakoshushwa shehena yake.

Hata hivyo inatajwa, bado suala la kusambazwa mafuta ni shida, kutokana na uhaba wa visima vya mafuta hasa kwa maeneo ya vijijini unaowafanya wenye magari, malori au mabasi ya abiria na magari madogo, walazimike kujaza mafuta mengi kuwafikisha vijijini na kurudi.

EWURA imekuwa ikihamasisha sekta binafsi kujenga vituo vya mafuta katika maeneo ya vijijini na kutoa unafuu katika leseni, kwani ujenzi wa huko ni gharama kubwa.

Mbali na hali hiyo sekta binafsi inatajwa kusuasua kuwekeza, hivyo kutokana na ombwe hilo, TPDC imeamua kuweka visima 100 vijijini.

### UWEKEZAJI MPYA ULIVYO

Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dk. James Mataragio anasema, ndani ya miaka mitano ijayo watashirikiana na halmashauri za wilaya kujenga vituo 100 vya mafuta katika maeneo ya vijijini.

Anasema, asasi hiyo imebaini kuwa vituo vingi vya mafuta nchini vimejengwa mijini na vinaendelea kujengwa huko, hivyo hatua yao ya kujenga vituo 100 vijijini itasukuma maendeleo vijijini.

Mpaka sasa anataja TPDC imeshajenga visima vya mafuta katika mikoa ya Tanga, Mara, Singida, Geita na Manyara lakini vinavyofanya kazi ni vya Segera, Tanga na cha Tarime mkoani Tanga.

Dk. Mataragio anasema vituo vitatu zaidi vitakarabatiwa mwaka huu wa fedha vya Makuyuni, Manyara, Singida na Geita. Anaendelea: “Tunataka kuwafikia wananchi wote na tumeona umuhimu wa kutoa huduma hii ya mafuta katika maeneo ambako haipo. “

Anafafanua kuwa TPDC inatekeleza mradi huo kupitia kampuni yake tanzu ya TANOIL, ambayo Meneja Mkuu, Kapulya Musomba, anasema wamepiga hatua kufungua vituo vya kuuza petroli Tanga, Mara, Geita, Singida na Manyara.

Anasema rekodi za mauzo kati ya Machi na Julai, 2021 zinaonyesha lita milioni 26 za mafuta ziliuzwa ikiwa ni wastani wa lita milioni 5.2 kwa kila mwezi, hivyo vituo vipya 100 vitawasaidia kupenya katika soko la vijijini na hivyo kuingiza mapato zaidi.

Kwa mujibu wa Musomba, biashara waliyofanya kwa miezi hiyo mitano, wameweza kulipa kodi ya Sh. bilioni 17.9 na wana mpango wa kuongeza tija na wateja kupitia promosheni za masoko.

Meneja Mkuu anaeleza imani yake kwamba, wana uwezo wa kuhimili ushindani wa kuuza mafuta yao kwa bei ndogo, lakini itakayowawezesha kupata faida.

Musomba anasema, katika kulinda usambazaji mafuta na bidhaa zake nchini, watafuata taratibu za kuuza bidhaa zenye ubora, ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi mafuta, kutangaza bidhaa yao na ufanisi.

Anasema kama ilivyo kwa biashara nyingine, wanakabiliwa na uhaba wa miundombinu ya kuhifadhi mafuta, soko lisilotabirika na ushindani mkubwa.

Anaahidi wataendelea kuboresha huduma zao, kwa kuongeza ufanisi, umakini na umahiri katika utoaji wa huduma za mafuta na bidhaa zake, ili waweze kufikia malengo waliyojiwekea.

Ni namna ambayo EWURA inajipanga kudhibiti bei ya mafuta katika maeneo yote, kwa kuwa kila sehemu itakuwa inauza mafuta kwa bei halisi na yenye faida.





## Wataka TAKUKURU kuchunguza mashine

Na Renatha Msungu, CHAMWINO

WAKAZI wa Kijiji cha Chenene wilayani Chamwino mkoani Dodoma wameiomba Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Tanzania (TAKUKURU) kuingilia kati suala la ununuzi wa mashine ya kupampu maji ya kijiji hicho kutokana na ubadhirifu unaofanywa.

Takribani mwezi na nusu sasa, wanakijiji wa Chenene wanafuata huduma ya majisafi na salama umbali mrefu huku wakihofia kuhatarisha maisha yao.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara kijijini, hapo momoja wa wakazi hao, Julius Jonas, alisema kero hiyo imekuwa ya muda mrefu, lakini hakuna ufumbuzi wowote unaofanywa.

Jonas alisema maji wanayochota si salama hivyo kuna hatari ya kutokea magonjwa ya mlipuko kwa wakazi wa kijiji hicho.

Kutokana na hilo alisema wanaiomba TAKUKURU kufanya uchunguzi wao ili waweze kuwabaini wanaokwamisha ununuzi wa mashine hiyo kwa maslahi yao binafsi.

Alisema tatizo la maji limekuwa sugu, hivyo wanahitaji msaada wa serikali kuhakikisha maji yanapatikana kijijini hapo.

Kadhalika alisema wanakijiji wako tayari kutoa ushirikiano wowote ili kuhakikisha wanapata majisafi na salama.

Naye Mwenyekiti wa Kijiji cha Chenene, Albert Chitung'ati, alisema wanaomba Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kushughulikia suala la maji katika kijiji hicho sababu imekuwa kero kubwa kutokana na wao kufuata maji umbali mrefu na kwa gharama kubwa.

Alisema mashine ya kupampu maji iliyonunuliwa ina uwezo mdogo hivyo maji hayatoki kwa muda wa miezi mingi sasa na kwamba wanawake wamekuwa wakitoka usiku wa manane kwenda kutafuta maji hivyo wamekuwa wakihofia usalama wao.

Pia alisema kero hiyo imekuwa ya muda mrefu, hivyo wanaiomba serikali kuingilia kati suala hilo.

Alifafanua kuwa lengo lao ni kuona maji yanatoka ili waweze kupata huduma ya majisafi na salama katika kijiji hicho.

# Waratibu maabara wa halmashauri wanolewa

Na Paul Mabeja, DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Bodi ya Maabara Binafsi imeendelea kutoa mafunzo kwa waratibu wa huduma za maabara ngazi ya halmashauri.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa namna bora ya kusimamia na kuboresha huduma zinazotolewa na maabara binafsi za afya nchini.

Mafunzo hayo ya siku tatu yanayoendelea jijini Dodoma, yalifunguliwa juzi Msajili wa Maabara Binafsi za Afya kutoka Wizara ya Afya, Dominic Fwiling'afu aliyemwakilisha Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe.

Fwiling'afu alisema utoaji wa huduma za afya kwa wananchi, mwaka 1997 serikali ilipitisha sheria sura 136 ya kusimamia utoaji wa huduma za maabara binafsi za afya.

Alisema lengo ni kuhakikisha huduma zinatolewa na maabara binafsi za afya zinakidhi vigezo na kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.

"Katika jitihada za kuimarisha upatikanaji na utoaji huduma za afya kwa wananchi, mwaka 1997 serikali ilipitisha sheria sura 136 ya kusimamia utoaji wa huduma za maabara binafsi za afya ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa viwango vinavyotakiwa," alisema.

Msajili alisema katika mafunzo hayo, waratibu watapitishwa kwenye changamoto mbalimbali zilizobainika kwenye ukaguzi uliofanywa na bodi kwenye mikoa mbalimbali na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzitatua ili kuboresha utekelezaji wa majukumu.

Pia alisema mafanikio yatakayopatikana baada ya kikao hicho yatasaidia kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa huduma bora za afya nchini kwa kuwa masuala ya maabara yana umuhimu wa pekee katika kutambua vyanzo vya magonjwa na matibabu yake kisayansi.

"Mafunzo haya yakawe chachu kwenu kuhakikisha maabara binafsi zote mnazosimamia zinatoa huduma zenye viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo yote inayotolewa na wizara inayohusu uanzishwaji na usimamiaji wa huduma bora za maabara binafsi za afya ili wagonjwa wapate tiba sahihi na kwa wakati," alisisitiza.

Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Dawa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Matthew Mganga, aliwataka waratibu wa maabara wa halmashauri kuwa kichocheo cha kukuza taaluma ya huduma za maabara ili wananchi wapate huduma bora na kwa wakati, hali itayoijengea taswira nzuri serikali inayosimamia huduma hizo.

Pia aliwataka wataalamu hao kusimamia utoaji huduma za maabara kwa kufuata kanuni, miongozo, taratibu na sheria za utoaji huduma za maabara bila kumwonea mtu ili kuondoa kero na malalamiko kuhusu huduma kutoka kwa wananchi.



Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Nhonge, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dodoma jana, alitoa wito kwa wananchi kulipa kodi ya ardhi kabla ya mwaka kuisha ili kuepuka kutozwa faini au kupelekwa mahakamani. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkesha mkubwa kuliombea taifa leo

Na Peter Mkwavila, DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, anatarajiwa kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mkesha mkubwa wa kitaifa wa kuukaribisha Mwaka Mpya utakaofanyika leo jijini hapa.

Hayo yalibainishwa jana na Mwenyekiti wa Taifa wa Mkesha huo wa dua maalumu, Askofu Mkuu wa Tanzania Fellowship of Churches (TFC), Dk. Godfrey Malassy.

Alisema kwenye mkesha huo, maombi mbalimbali yatafanyika, ikiwamo ya kuliombea taifa la Tanzania ili Mungu aliponya liondokane na hofu inayosababishwa ugonjwa wa corona.

Dk. Malassy alisema mkesha wa mwaka huu ambao unafanyika kwa mara ya kwanza makao makuu ya nchi, una lengo la kumwombea Rais Samia pamoja na wasaidizi wake.

Aliwaomba Watanzania kuitumia siku hiyo kufanya maombi na dua maalumu kwa ajili ya kuliombea taifa amani na utulivu wakiwamo viongozi wa kitaifa.

Kwa mujibu wa Malassy, wajibu wa kila Mtanzania ni kuhakikisha anaomba kwa ajili ya nchi yake ikiwa na pamoja kuwaombea viongozi wake ili taifa liishi kwa amani na utulivu.

Kuhusu maandalizi ya mkesha huo, alisema Watanzania wanatakiwa kuendelea kufanya maombi hasa katika kipindi ambacho dunia inakabiliana na ugonjwa wa corona.

"Mkesha huu unajumuisha watu wote bila kujali imani za kidini, itikadi za kisiasa kwa kuwa lengo kuu ni kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea kuwapo, ikizingatiwa kuwa bila hivyo hakuna jambo lolote linaloweza kutendeka," alisema.

Naye Lucas Mbise, akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwaomba Watanzania watakaofika katika maombi kuweka nia zao thabiti kwa Mwenyezi Mungu ili kuweza kujibiwa mahitaji yao.





# Wamiliki mabasi waonywa upandishaji nauli holela

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imewaonya wamiliki wa mabasi wanaopandisha nauli holela kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka na kuwataka waache ili kuepuka kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alitoa tahadhari hiyo jana alipofanya ziara ya kushtukiza kwenye Kituo Kikuu cha Mabasi cha Mkoa wa Mbeya na kukagua tiketi za abiria, kuzungumza nao na kutoa maagizo mbalimbali.

Waitara alisema kabla ya mmiliki wa basi kupewa leseni ya kusafirisha abiria, anapatiwa elimu, nakala ya sheria na kanuni za usafirishaji ambazo ndizo zenye miongozo ya namna ya kupandisha nauli na kushusha.

Alisema ili kufanya mabadiliko ya nauli za mabasi, lazima kifanyike kikao cha wadau wa usafirishaji kikiwamo Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini.

Kwa sasa, alisema hakuna kikao chochote ambacho kimefanyika na kufanya mabadiliko ya nauli za mabasi lakini kuna baadhi ya wamiliki wameanza kupandisha nauli kienyeji hasa kipindi hiki ambacho abiria ni wengi.

"Nawashukuru watu wa Mbeya, nimekagua mabasi karibia yote yanayoenda Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Arusha sijaona abiria yeyote anayelalamika kupandishiwa nauli. Nawapongeza sana lakini nawashauri mwendelee hivi hivi," alisema Waitara.

Alisema ukaguzi huo ulianzia katika Kituo Kikuu cha Magufuli mkoani Dar es Salaam na baadaye Arusha, Mwanza ambako wamiliki walitozwa faini na wiki hii ameamua kufanya ziara Mbeya kujiridhisha kama watu wanazingatia sheria.

Waitara alisema kwa mujibu wa sheria za usafirishaji, mmiliki wa basi akikutwa anazidisha nauli anatozwa faini ya kati ya Sh. 200,000 na 500,000 au kwenda jela kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja ama vyote viwili.

Alisema wakati wa kubadili nauli huwa vinaangaliwa vigezo mbalimbali ikiwamo ongezeko la bei ya mafuta, gharama za vipuri na gharama zingine za uendeshaji.

Baadhi ya mawakala wa mabasi katika kituo hicho walisema kipindi hiki abiria ni wengi tofauti na miezi mingine lakini wanaogopa kupandisha nauli kwa sababu ukaguzi unafanyika mara kwa mara na LATRA pamoja na mamlaka zingine.

Justine Mdolo, wakala wa mabasi ya Premier yanayofanya safari kati ya Mbeya na Mwanza, alisema wakati mwingine nauli huwa zinapandishwa na wapigadebe ambao huwa wanajitafutia kipato.

Aliwataka abiria kuacha kuwapa fedha wapigadebe na badala yake wawe wanaingia kwenye ofisi za kampuni husika ili kuepuka kuibiwa kwa kuwa wapigadebe hao huwa wanawasilisha fedha kulingana na nauli za mabasi husika, lakini fedha wanazoongeza zinakuwa zao.

"Tunawashauri abiria wawe wanaingia kwenye ofisi za mabasi badala ya kuandikiwa tiketi barabarani. Sisi tunaweza tukaonekana wahuni lakini tukibaini kwamba abiria amefanyiwa uhuni huwa tunawabana mpaka wanarejesha fedha za abiria," alisema Mdolo.



Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson (wapili kulia), akikata utepe juzi kuzindua nyumba ya mtoto anayepumulia mashine, Steven Shaban, ambayo imejengwa na wasamaria wema katika Mtaa wa Nonde jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wananchi waongezeka chanjo corona

**Na Nebart Msokwa,** ILEJE

IDADI ya wananchi wanaojitokeza kupata chanjo ya corona katika wilaya ya Ileje mkoani Songwe, imeongezeka baada ya serikali kuanzisha kampeni maalumu ya mpango harakishi na shirikishi.

Mratibu wa Huduma za Chanjo wa Mkoa wa Songwe, Moses Lyimo, aliyasema hayo juzi wakati wa kampeni wilayani hapa na kubainisha kwamba kampeni hiyo na zile zilizofanyika awali, zimeongeza uelewa miongoni mwa wananchi.

Alisema watu wengi walikuwa wanapinga chanjo, sasa wamehamasika na wameanza kujitokeza kuchanjwa na kwamba mpango huo una mafanikio kwa sababu unawashirikisha viongozi wa ngazi za mitaa.

Lyimo alisema kabla ya kampeni hiyo, watu wengi walikuwa wanapinga lakini baada ya serikali kutekelezwa kwa kampeni ya kwanza na ya sasa, watu wengi wameanza kuamini chanjo na wanajitokeza kuchanja.

Mratibu wa Huduma za Chanjo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, Innocent Charles, alisema Mpango Harakishi na Shirikishi wa awamu ya pili umekuwa na manufaa zaidi kwa sababu unawashirikisha watoa huduma ngazi ya jamii.

Alisema watoa huduma hao wanashiriki kuwahamasisha wananchi kuchanja huku na wao wakiwa mfano kwa kuwa wa kwanza kuchanja na kuwaaminisha wananchi.

Pia alisema wananchi wanaelimishwa na kuamua wao wenyewe kwa hiari kuchanja na kwamba kwa sasa kazi ya kutoa elimu sio ngumu kama ilivyokuwa awali wakati huduma hiyo inaanza.

"Tunashukuru kwa sasa kazi sio ngumu ya kuwahamasisha wananchi, wengi wanajitokeza baada ya kuelewa umuhimu wa chanjo, mpaka sasa huduma hii ni hiari ya mtu mwenyewe lakini kinachotakiwa ni elimu tu kwa wananchi," alisema Charles.

Kiongozi wa Timu ya Uhamasishaji Wananchi kupata chanjo ya corona, kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Subisya Kabuje, aliwataka wananchi kujitokeza kuchanja ili kuwa salama.

Aliwataka viongozi wa halmashauri zote za mkoa wa Songwe kuhakikisha wanashiriki kuhamasisha watu kujitokeza kuchanja pamoja na kuhakikisha usahihi wa chanjo.

Songwe ilikuwa miongoni mwa mikoa ambayo ilikuwa na idadi ndogo ya watu waliokuwa wanajitokeza kuchanja lakini baada ya kampeni, takwimu zimepanda na hata idadi ya wanaojitokeza kwa siku imefikia zaidi ya watu 40 kwa siku.

## Walia hali ngumu usafiri barabara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Ikombe Kata ya Matema wilayani Kyela, wameiomba serikali iwajengee barabara ya kuunganisha kijiji hicho na makao makuu ya kata ili waondokane na usafiri wa kutumia mitumbwi ambayo inahatarisha maisha yao.

Wananchi hao walisema juzi kuwa wanashindwa kupata huduma muhimu ambazo zinapatikana Matema na hata kuvuka kwenda kupata huduma Kyela mjini na maeneo mengine ya mkoa wa Mbeya kwa sababu ya kukosa barabara.

Mmoja wa wananchi hao, Julius Angumbwike, alisema walijaribu kuchimba barabara kwa kutumia jembe la mkono, lakini walikwama kutokana na jiografia ya eneo hilo kuwa na milima na mawe makubwa ambayo yaliwaletea shida.

Alisema barabara hiyo waliichimba pembezoni mwa Ziwa Nyasa na serikali iliwaahidi kuikamilisha barabara hiyo lakini mpaka sasa haijatekeleza.

"Sisi huku biashara yetu kubwa ni vyungu na samaki, lakini wateja wetu wako Kyela na Mbeya. Sasa huwa tunalazimika kusafirisha kwa kutumia mitumbwi kwa sababu magari hayawezi kufika hapa," alisema Angumbwike.

Alisema hata uchumi wao unashindwa kukua kwa sababu ya kukosekana kwa usafiri wa uhakika na hivyo akaiomba serikali iwasaidie ili kukifungua kijiji hicho.

Mbunge wa Kyela, Ally Jumbe, alisema alifanya ziara katika kijiji hicho akiwa ameambatana na maofisa wa Wakala wa Barabara (TANROADS) kwa ajili ya kuangalia namna ya kujenga barabara hiyo.

Alisema tatizo la barabara hiyo ni kwamba kuna milima yenye miamba mingi ambayo inatakiwa kupasuliwa kwa kulipuliwa na baruti pamoja na kuboresha madaraja na kwamba kuna mkandarasi alitakiwa aijenge barabara hiyo lakini aliitelekeza.

Jumbe alisema barabara hiyo ni muhimu kwa wananchi wa kijiji hicho kwa sababu kina wananchi wa eneo hilo wanapata huduma muhimu katika maeneo ambayo wanalazimika kupita kwenye maji.

Alisema barabara hiyo na zingine za Kyela mjini ziko kwenye mipango ya serikali kujengwa, hivyo akawataka wananchi kuwa wavumilivu wakati harakati za ujenzi zikiendelea.

**Alisema barabara hiyo waliichimba pembezoni mwa Ziwa Nyasa na serikali iliwaahidi kuikamilisha barabara hiyo lakini mpaka sasa haijatekeleza.**



## Serikali yapiga marufuku kuvua samaki kasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imewataka wavuvi kuacha kuvua samaki aina ya kasa kwa sababu hawapo salama kutokana na tishio la mabadiliko ya vyakula wanavyokula na kusababisha sumu ya mwili ambayo matokeo yake ni kifo kwa binadamu anayekula nyama yake. Hayo yalisemwa na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Abdalla Hussein Kombo, wakati akitoa taarifa ya maendeleo ya wizara hiyo katika sekta ya uvuvi na uchumi wa bluu.

Alisema utafiti mdogo uliofanywa, umebaini kasa wanakula chakula aina ya majani yenye mchanganyiko wa sumu na nyama yake akila binadamu husababisha kifo.

Alisema matukio ya vifo vya wananchi mbalimbali mwishoni mwa mwaka huu na mwaka jana vimeitia hofu serikali na kuja na tamko la kuwataka wavuvi kuacha kuvua samaki hao.

Alisema serikali kwa muda mrefu inatekeleza tamko la kimataifa la kupiga marufuku uvuvi wa kasa kutokana na viumbe hivyo kuwapo katika tishio la kutoweka.

"Kasa tayari wameingizwa katika orodha ya viumbe ambavyo vipo katika tishio la kutoweka na ndiyo maana uvuvi wake umepigwa marufuku duniani kote," alisema.

Waziri Kombo alisema tayari katika kipindi cha mwezi mmoja jumla ya vifo vya wananchi waliokula kasa ikiwamo watoto kufikia 17.

"Tumeshuhudia vifo vya watu 14 huko Tumbe, Pemba kwa kula kasa na hivi karibuni tumeshuhudia vifo vya watu watatu kwa kula samahi huyo huko Matemwe Unguja ikiwamo watoto wadogo ambapo inaonyesha wavuvi wamekuwa wakivua samaki hao kwa wingi kwa matumizi ya kula na biashara," alisema.

Aidha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, alizitembelea familia za watu walioathirika na kula nyama hiyo na kusababisha watu wanne wakifariki dunia huko Matemwe, kwa ajili ya kuwapa pole. Alisema wavuvi wote wanafahamu kwamba wapo aina ya kasa ambao ni marufuku kwa matumizi ya kula, lakini imebainika wapo wengine ambao wanaliwa, lakini katika mabadiliko yaliyopo sasa pia wamekuwa na kasoro ya sumu.

"Niliwauliza kasa mwenye sumu anafahamika vizuri kwa wavuvi wote wenye uzoefu sasa nyinyi huyu aliyevuliwa na kuliwa alikuwa wa aina gani, walijibu alikuwa salama, lakini amesababisha kifo huku wakiwa na wasiwasi kwamba atakuwa amekula aina fulani ya majani yenye sumu," alisema.

Mtaalamu aliyebobea katika masuala ya viumbe vya bahari ambaye alifanya kazi katika Taasisi ya Sayansi ya Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Narman Jidawi, alisema kasa anapokuwa baharini chakula chake kikubwa ni aina mbalimbali za majani ikiwamo mwani.

"Kasa wakati mwingine anakula majani ya aina mbalimbali mengine hugeuka sumu ambayo kwake yeye haina madhara, lakini kwa binadamu akila nyama hiyo husababisha kifo," alisema. .

# Watumiaji bodaboda, bajaji wapewa elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, amesema sekta ya usafiri wa bodaboda na bajaji ni mpya kwa Zanzibar na kwamba kuna haja ya kutoa elimu ya matumizi bora ya barabara hususan kwa madereva na watumiaji wa huduma hiyo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa waendesha bodaboda katika viwanja vya Mao Zedong mjini hapa yaliyoandaliwa na Shirika la Bima Tanzania.

Alisema usafiri huo umerasimishwa rasmi Zanzibar kwa mujibu wa sheria na matumaini yake ni kuwa washiriki wa mafunzo hayo watapata fursa ya kueleweshwa undani wa sheria na kanuni zake pamoja na kujikinga na majanga yatokanayo na ajali za barabarani.

"Elimu hii itasaidia kuepusha madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya barabara na vyombo vya moto," alisema.

Aliipongeza jumuiya ya bodaboda kwa kujipanga na kusimamia uundwaji wa jumuiya yao ambayo ni kiunganishi kikuu baina ya serikali kupitia idara husika na waendesha bodaboda katika kuweka mazingira bora ya utendaji kazi, usalama wa raia na taifa kwa ujumla.

Alisema aina hiyo ya usafiri ina changamoto nyingi hususan kwa madereva, abiria na watumiaji wa barabara na nyingi zinahusu ukiukwaji wa sheria na miongozo mbalimbali ya matumizi bora ya barabara kwa vyombo vya moto.

Pia alisema katika utekelezaji wa sheria na kanuni za usafiri barabarani, bima na zingine aliziagiza taasisi husika kusimamia vyema utekelezaji ili taifa lipunguze engezeko la ajali za barabarani, vifo na majeraha yanayotokana na ajali za barabarani, hasara za hali na mali kwa waathirika wa ajali.

Naye Ofisa Mnadhimu wa Kikosi cha Usalama wa Barabarani, Mkadam Khamis Mkadam, aliwataka madereva hao kufuata sheria za usalama barabarani ili kupunguza madhara.

Alisema kazi ya kusafirisha abiria kupitia usafiri wa bodaboda ni kazi zingine na kuwataka kuithamini kazi hiyo na kuwa wasafi na watanashati ili kazi yao ikubalike katika jamii.

Mkadam ambaye Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi, alisema kuwa elimu hiyo wanayoitoa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwataka wasiwe wakamataji, pia watoe elimu kwa makundi yote ya watumiaji wa barabara.

Kwa upande wake Kamishna wa Bima kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Mussa Juma, alisema wametoa elimu hiyo ili madereva hao kujua madhara wakati ajali inapotokea kwa kuokoa maisha yao na abiria wao.

Madereva waliopatiwa mafunzo hayo walisema kuwa watahakikisha elimu waliyopatiwa wanaifanyia kazi na kuwataka madereva wenzake kuhakikisha wanafuata sheria za barabarani ili kupunguza ajali.



Mkuu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Zanzibar, Komodoo Azan Hassan Msingiri, akizungumza na maofisa na wapiganaji wa kikosi hicho, Kibweni Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Vyombo vya sheria vyatakiwa kushirikiana

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JAJI wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Ibrahim Mzee Ibrahim, amevitaka vyombo vya sheria kushirikiana kuzipatia ufumbuzi kesi mbalimbali zinazowakabili wananchi na kupata hukumu yake kwa wakati.

Aliyasema hayo wakati alipokutana na wadau wa sekta wa vyombo vya sheria kwa ajili ya kujitambulisha kufuatia kuteuliwa kuwa Jaji Mkazi wa Mahakama Kuu Pemba huko Chakechake, Pemba.

Alisema malengo ya kuchaguliwa kwake kushika wadhifa huo kwa upande wa Pemba ni kusikiliza kesi zinazowakabili wananchi ikiwamo za Mahakama Kuu kwa wakati na kutoa hukumu yake.

Alisema ushirikiano na vyombo vya sheria vinavyosimamia mwenendo wa makosa ya jinai ikiwamo Mahakama, Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kufanya kazi kwa pamoja ni muhimu na kuibua changamoto zote kikwazo katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.

"Nimechaguliwa kuwa Jaji Mkazi katika kisiwa cha Pemba kwa ajili ya kusikiliza mashauri ya wananchi kwa kasi kufuatia malalamiko ya muda mrefu ya mahitaji ya Jaji Pemba," alisema.

Aidha, Mkurugenzi wa Mashtaka, Salma Ali Hassan, alisema, ushirikiano mzuri wa mahakama na ofisi yake utafanikisha malengo ya Serikali ya Zanzibar kusikiliza kesi za udhalilishaji kwa kasi na kutolewa hukumu.

"Tumetakiwa tufanye kazi kwa pamoja na ushirikiano hatua ambayo itasaidia kuzipatia ufumbuzi changamoto za sheria na kesi kusikilizwa kwa wakati," alisema.

Akizungumza kuhusu uteuzi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema uamuzi wa kuwapo kwa Jaji Mkazi Pemba ni miongoni mwa kilio cha muda mrefu cha viongozi mbalimbali wakiwamo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa upande wa Pemba kuona anakuwapo jaji atakayesikiliza kesi zenye hadhi ya Mahakama Kuu kwa haraka.

Alisema baadhi ya kesi zitakazoshughulikiwa na Jaji ni zinazohusu matukio ya makosa ya jinai ikiwamo tuhuma za mauaji ambazo huchukua muda mrefu kwa sababu ya kutokuwapo kwa Jaji Mkazi.

"Hizo ndiyo sababu zilizosababisha kuwapo kwa Jaji mkazi Pemba...ni kilio cha muda mrefu cha viongozi na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kinachotokana na kusikilizwa kwa kesi haraka za jinai zinazowakabili watuhumiwa mbalimbali ambao hukaa rumande muda mrefu kusubiri jaji atoke Unguja kusikiliza kesi," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA MOROGORO MJINI MASIKA MIL. 100. NI NZURI KWA BIASHARA, INA VYUMBA KUMI NA NNE. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU NAMBA**: **0745 222 312 / 0715 768 811.**

## KIWANJA KIANUZWA.

KIWANJA KIANUZWA KISUKURU JKT KIWANJA KIPO KISUKURU JKT SEGEREA UKUBWA SQM 2252 KINA HATI BEI MILIONI 55, **KWA MAWASILIANO: 0786 857523 AU 0655 857523**

## NAFASI ZA UALIMU

NAFASI ZA KAZI YA UALIMU DIPLOMA AU DIGRII YA KIINGEREZA,HESABU NA SCIENCE CHEKECHEA NA DARASA LA 6 NA 7 **SIMU: 0783298900**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



**ANNA WAMBURA MBAGE** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cheti cha **KIDATO CHA NNE** chenye namba za usajili S 1706/0002/2010 kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia **PASIANSI SEKONDARI mwaka 2010, CHETI CHA KUZALIWA, TECHNICAL CERTIFICATE IN FISHERIES SCIENCE AND TECHNOLOGY** kilichotolewa na chuo cha **FISHERIES EDUCATION TRAINING AGENCY** mwaka **2014** na **TRANSCRIPT** yake, **ORDINARY DIPLOMA IN FISHERIES SCIENCE AND TECHNOLOGY** kilichotolewa na chuo cha **FISHERIES EDUCATION TRAINING AGENCY** mwaka **2015 na RESULT SLIP** yake.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa yapolisi: **REF/GE/TR/RB/6090/2021.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamiziwa mirathi Na 117, 2021**
**Katika shauri la mirathi ya ANTONY JUSTINE RWEYENDELA.....Marehemu**
**Wa NJOMBE**
**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na BEATRICE OBEDY LEKASIO ......Mwombaji.**

**TANGAZO KWA UMMA.**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **...29.......mwezi ...01..... mwaka... 2022.....** kabla ya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo ,mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe...29.... mwezi ...12.... **Mwaka...2021.....**

HAKIMU MKAZI

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 74 OF 2021**

In the Matter of the Estate of the Late **FRANCIS SAMSON NGALAWA**

**By 1. LYDIA MPONZI NJEJE**
**2. ……………………………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above −named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 11 day of JAN.. 2022

**Dated at MOROGORO this 29 day of DEC………2021**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MICHAEL ALLAN KIJAZI** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T772DXN, TOYOTA HAICE** Engine **No. 1KD2708080** Chassis **No.JTFST22P300031854** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi . Taarifa ya polisi **ARU/ARU/RB/609000/2021.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASASI**
**Kituo cha LISEKESE Mkoa wa MTWARA**
**Shauri la Madai / Ndoa Na. 75/2021**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

Kwa: SAMWEL ANDREA ZEBEDAYO – MKAZI WA KARATU ARUSHA

K.K. MTENDAJI WA MTAA (KIJIJI)
Kwa kuwa mdai / wadai ameleta / wameleta madai yake / yao kwamba / Eleza hapa habari ya madai

**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 01 Mwaka 2022 saa 08:30 asubuhi / mchana kwa mujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako / wenu na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 07 Mwezi 12 Mwaka 2021.

Hakimu
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO LISEKESE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TAHER KARIMJEE BADRUDDIN** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T244CJQ, SUBARU IMPREZA.** Engine **No. EJ205DW6BE.** Chassis **No. GDAD48D.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi **ARU/ARU/RB/609003/2021.**

Uza, Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Ethiopia kuanza na tume ya majadiliano kitaifa

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

WABUNGE wa Ethiopia, wamepitisha muswada, utakaoidhinisha kuundwa kwa tume ya mazungumzo ya kitaifa, kufuatia shinikizo la kimataifa la kuwapo kwa mazungumzo hayo, yanayonuiwa kumaliza vita vya miezi 13 katika jimbo la Tigray.

Bunge la shirikisho, lilipiga kura kuidhinisha muswada huo kwa kura 287, huku kura 13 zikiupinga na moja kutopigwa kabisa.

Kuundwa kwa tume hiyo kutafungua njia ya majadiliano ya kitaifa na kukuza uaminifu wa taifa.

Serikali ya Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, iliahidi kuunda tume hiyo, ili kuwa na mahala pa kujadili masuala yanayoleta utata.

Hata hivyo tume hiyo kwa sasa haitolijumuisha kundi la TPLF wala Jeshi la ukombozi la Oromo katika majadiliano.

Makundi yote mawili yanapambana na jeshi la Ethiopia na yalitangazwa kuwa makundi ya kigaidi na serikali ya taifa hilo la Afrika Mashariki.

Kuundwa kwa tume, huenda kukawa ni juhudi ya Ethiopia, kujibu shinikizo kutoka kwa jamii ya kimataifa kutaka mapigano yasitishwe na mazungumzo ya kutafuta suluhu ya kudumu kwa mvutano uliopo.

Tsedale Lemma, Mkurugenzi wa chombo kimoja cha habari Ethiopia, alisema wakati jamii ya kimataifa ilipopendekeza kuwapo kwa mazungumzo ya kitaifa, ilimaanisha kujumuishwa kwa makundi yote kuwa sehemu ya mchakato wa upatikanaji wa amani, kwa sasa serikali ya Ethiopia ina sera ya kutojadili chochote na makundi yaliojihami.

Tsedale Lemma, alisema iwapo hilo litafanyika, itakuwa ni juhudi ya serikali kuunda tume ambayo haina nia yoyote ya kutatua mgogoro wa kisiasa unaoikumba nchi hiyo.

**DW**

# Mwili wa Desmond Tutu waagwa, kuzikwa kesho

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

MWILI wa Askofu Mkuu Desmond Tutu umewasili jana katika Kanisa Kuu la St. George mjini Cape Town, utalala kwa siku mbili kwa heshima ya mazishi kitaifa.

Tutu, mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel, ambaye alisaidia kukomesha ubaguzi wa rangi nchini Afrika Kusini, alifariki Jumapili akiwa na umri wa miaka 90.

Mazishi yake rasmi ya kiserikali yatafanyika kesho, baada ya kuruhusu waombolezaji kuupita mwili wake na kuuaga kwa mara ya mwisho kwa siku mbili.

Muda wa kulazwa katika kanisa hilo ulilazimika kuongezwa hadi siku mbili, kuhofia kutokea mkanyagano, kasisi wa eneo hilo aliliambia shirika la habari la AFP.

Mapadre walichoma uvumba wakati jeneza la Tutu la misonobari, likiwasili ndani ya kanisa kuu.

Mjane wa Tutu, Leah, alitembea nyuma polepole wakati jeneza likiingia katika parokia yake ya zamani.

Umma ulitoa heshima zao kwa kiongozi huyo wa kidini anayeheshimika sana, nguzo muhimu katika mapambano ya kukomesha mfumo wa ubaguzi wa rangi uliotekelezwa na serikali ya wazungu wachache dhidi ya weusi walio wengi Afrika Kusini, kuanzia mwaka 1948 hadi 1991.

Ibada za ukumbusho zitafanyika kote Afrika Kusini, huku usiku wa ukumbusho na marafiki wa karibu ukifanyika baadaye.

Baada ya mazishi ya kesho, mabaki ya Tutu yatachomwa na majivu yake kuwekwa katika kanisa kuu, ambako alihubiri kwa miaka mingi.

Kengele za kanisa kuu hilo zimekuwa zikilia kwa dakika 10 kila siku, saa sita mchana tangu kifo chake. **BBC**



Watoto wa Desmond Tutu, Mchungaji Nontombi Naomi Tutu na Thandeka Tutu, wakitazama jeneza la baba yao likiwasili Kanisa la St George, mjini Cape Town, nchini Afrika Kusini, jana. **PICHA: REUTERS**

# Rais Ghani asimulia kuitoroka Afghanistan

**Kabul,** AFGHANISTAN

RAIS wa zamani wa Afghanistan, ametetea uamuzi wake wa kutoroka nchini Taliban walipokaribia kuuteka mji mkuu Kabul, mapema mwaka huu.

Amesema alifanya hivyo kuzuia uharibifu wa Kabul.

Taliban waliingia madarakani Augosti, mwaka huu, baada ya kuchukua udhibiti wa mji mkuu.

Ashraf Ghani, alifichua jinsi alivyoamka asubuhi ya Agosti 15 bila kujua itakuwa siku yake ya mwisho Afghanistan.

"Ni pale ndege ilipoondoka Kabul ndipo niligundua kweli naenda zangu," Ghani aliambia Kituo cha BBC Radio 4.

Alikosolewa vikali na kulaumiwa kwa kutoroka nchi, wakati huo. Sasa anaishi Umoja wa Falme za Kiarabu, (UAE).

Ghani alitoa tamko hilo, wakati wa mazungumzo yake na Jenerali Sir Nick Carter, Mkuu wa zamani wa Majeshi ya Ulinzi wa Uingereza, ambaye alikuwa mhariri msaidizi wa kipindi hicho jana.

Ghani anakumbuka, wapiganaji wa Taliban ambao walikuwa wamekubali kutoingia Kabul, ingawa saa mbili baadaye walibadilika."Makundi mawili ya Taliban, yalianza kuingia mji huo kutoka pande mbili tofauti," Ghani alieleza.

"Na uwezekano wa kutokea mzozo mkubwa kati yao ambao ungeharibu mji wa milioni tano na kuleta maafa kwa watu ulikuwa mkubwa sana."

Alikubali kumruhusu mshauri wake wa usalama wa taifa na mkewe, kuondoka Kabul, kisha akasubiri gari la kumpeleka kwa wizara ya ulinzi.

"Gari halikuja. Badala yake, mkuu wa usalama wa rais aliyejawa na hofu alimjia na kusema kwamba ikiwa Bw Ghani atachukua msimamo wa kusalia madarakani, wote watauawa".

"Hakunipa zaidi ya dakika mbili," Ghani alisema.

"Maagizo yangu yalikuwa ni kujiandaa kwa ajili ya kuondoka kuelekea mji wa Khost. Aliniambia kwamba Khost ilikuwa chini ya Taliban pamoja na mji Jalalabad pia.

"Sikujua tutaenda wapi. Tulipoondoka tu, ikawa wazi kwamba tunaondoka [Afghanistan]. Kwa hivyo hii ilikuwa hatua ya ghafla."

Baada ya kuondoka, Ghani alikosolewa na baadhi ya Waafghanistan, akiwemo Makamu wake wa Rais, Amrullah Saleh, ambaye aliitaja hatua hiyo kuwa fedheha.

Madai kwamba, Ghani alikuwa amechukua kiasi kikubwa cha pesa pia yaliibuka, jambo ambalo alikanusha vikali, akikaribisha uchunguzi wa kimataifa ambao alisema ungesafisha jina lake.

"Nataka kusema bayana, sikutoka na fedha zozote nje ya nchi," alisema na kuongeza: Mtindo wangu wa maisha unajulikana na kila mtu. Ningefanya nini na pesa?"

Ghani alikiri makosa yalifanyika, ikiwa ni pamoja na kudhani kwamba, subira ya jumuiya ya kimataifa ingedumu.

Hata hivyo, aliashiria makubaliano yaliyofanywa kati ya Taliban na Marekani chini ya Rais wa wakati huo, Donald Trump, ambayo yalichangia matukio ya kuelekea Agosti 15, mwaka huu.

"Badala ya mchakato wa amani, tulipata mchakato wa kujiondoa," Ghani alisema.

Chini ya masharti ya makubaliano hayo, Marekani ilikubali kupunguza majeshi yake na yale ya washirika wake, pamoja na kutoa nafasi ya kubadilishana wafungwa, kundi hilo la wanamgambo lilikubali kufanya mazungumzo na serikali ya Afghanistan.

"Mapinduzi ya vurugu, si makubaliano ya kisiasa, au mchakato wa kisiasa ambao ulihusisha watu".

Siku hiyo hiyo, Ghani alipondoka Kabul, Taliban walichukua udhibiti. Tangu wakati huo, nchi hiyo imetumbukia katika mzozo wa kibinadamu na kiuchumi, ambao ulifanywa kuwa mbaya zaidi kwa kuondolewa kwa uungaji mkono wa kimataifa baada ya kundi hilo kunyakua mamlaka.

Miezi mitatu baadae, Ghani anasema yuko tayari kulaumiwa kwa baadhi ya mambo ambayo yalisababisha kutekwa kwa Kabul.

**BBC**

HABARI MICHEZO

# MAGORI AFUNGUKA KIBU STAA MPYA AJAYE NCHINI

**Na Adam Fungamwango**

MSHAURI wa Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Crescentius Magori, amesema kiwango anachokionyesha straika wa timu hiyo, Kibu Dennis ni dalili njema atakuwa mchezaji hatari na tegemeo katika siku za hivi karibuni.

Magori aliliambia gazeti hili uwezo wa Kibu ni mkubwa na endapo ataendelea hivi basi hatoshangaa kuona timu mbalimbali kubwa za barani Afrika zikianza kumnyemelea.

Kiongozi huyo alisema anamfahamu Kibu tangu alipokuwa akiichezea Geita Gold ilipokuwa inashiriki Ligi Daraja la Kwanza sasa hivi Championship na kupendekeza jina lake ndani ya Kamati ya Usajili na amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kumpa muda ili aendelee kujiimarisha.

Alisema Kibu anahitaji kupewa muda zaidi wa kuonyesha uwezo wake kwa sababu sasa hivi anaichezea Simba ambayo ni klabu kubwa, lakini ni mgeni pia kwenye Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara.

Aliongeza kwa sasa si Tanzania na Afrika, bali duniani kote huwezi kupata straika mwenye sifa zote za pamoja kama alizonazo mchezaji huyo ambaye ana stamina, kasi, uwezo wa kupiga mashuti ya mbali, kuweza kupiga miguu yote, kujituma na nidhamu.

"Ninamfahamu Kibu tangu yupo Geita Gold, wanachama na mashabiki wa Simba wasubiri mengi kwa mchezaji huyu, kuna vitu vidogo ambavyo vitamchukua muda, halafu ni kijana mdogo ana mengi ya kujifunza, pia amekuja kwenye timu kubwa kama Simba ambayo anawashinda hata wachezaji ambao wamecheza Ligi Kuu kwa muda mrefu," alisema Magori na kuongeza.

"Ni mchezaji anayeweza kupiga miguu yote miwili, anapiga mbali, ana nguvu, kasi, anajituma ana nidhamu kwa sasa siyo Tanzania au Afrika tu, duniani kumpata straika wa aina hiyo ni vigumu sana, anaweza kuwa na sifa hii, nyingine hana, na wengi wanafunga akiwa ndani ya boksi, wanaopiga mbali ni nadra sana duniani, huko tunakokwenda kwenye mechi za kimataifa kuna timu zinaweza kuanza kumfuatilia," Magori alisema.

Kibu ambaye hucheza kama winga, alijiunga na Simba msimu huu akitokea Mbeya City, na ameshafunga mabao manne akiwa Simba, matatu yakiwa ni kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Dirisha dogo Zanzibar Jumatatu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

DIRISHA dogo la usajili kwa wachezaji wanaoshiriki Ligi Kuu Zanzibar limepangwa kufunguliwa kuanzia Januari 3 hadi 20, mwakani, imeelezwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Hashim Salum, aliliambia gazeti hili usajili huo umepangwa katika kipindi ambacho ligi hiyo itakuwa imesimama ili kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Salum alisema usajili huo utahusisha timu zote za Ligi Kuu Zanzibar, Ligi Kanda ya Unguja, Ligi Kanda Pemba zote zitafanya usajili huo kwa njia ya mtandao kama ilivyokuwa wakati wa dirisha kubwa.

Kiongozi huyo amevitaka vilabu kuacha kufanya usajili huo kwa mazoea kwa kuheshimu kalenda hiyo ya usajili.

"Kikubwa timu zibadilike, twende na kasi iliyopo hivi sasa, wanaposikia dirisha limefunguliwa basi watumie muda huo kufanya usajili baada ya kusubiri muda wa ziada, tunawaambia mapema ZFF pamoja na Bodi ya Ligi hatutatangaza muda wa ziada," alisema Salum.

Alizipongeza timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar kwa kumaliza vyema mzunguko wa kwanza ambao unamalizika leo kwa ajili ya kuruhusu maandalizi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi.




Straika wa Fountain Gate Princess, Neema Paulo (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Yanga Princess, Fumukazi Ally, katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa wiki iliyopita. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

## Simba Queens yatamba haipoi

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema anaziheshimu timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu huku akiwanoa vyema wachezaji wake ili kiendelee kutoa 'dozi kubwa' katika mechi nyingine zinazofuata.

Simba Queens, ambao ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo watashuka dimbani Jumatatu kuwakabili Ilala Queens kwenye Uwanja wa Karume, Ilala jijini Dar es Salaam.

Nkoma alisema kufundisha timu inayoshiriki ligi hiyo ni mara yake ya kwanza, lakini kuwapa heshima wapinzani na kukiimarisha kikosi chake ndio siri ya kuendelea kuvuna matokeo chanya.

"Mimi ni mgeni kwenye ligi hii, sijawahi kufundisha klabu, hii ni mara yangu ya kwanza, naheshimu kila timu pinzani ninayokutana nayo, ninawaeleza wachezaji wangu wawe makini na kuhakikisha tunaendelea kutafuta idadi ya mabao mengi katika kila mechi," alisema Nkoma.

Kocha huyo aliongeza wamejipanga kupambana katika kila mchezo ili wafikie malengo ya kutetea ubingwa wanaoushikilia ambao unawaniwa na watani zao pia.

## Pamba yatangaza kutimua makocha

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba inayoshiriki Ligi ya Championship imetangaza kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Athumani Kairo pamoja na viongozi wengine wote wa benchi la ufundi akiwamo, kocha wa makipa, Emmanuel Kingu.

Uamuzi huo umechukuliwa kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo yenye makazi yake jijini Mwanza.

Mwenyekiti wa Mashindano wa Pamba FC, Aleem Bhai, alisema kamati yake imefanya uamuzi huo ili kuinusuru timu hiyo ambayo ilianza vyema msimu huu, lakini mambo yakaanza kwenda ovyo kadri siku zinavyozidi kusonga mbele.

Kiongozi huyo alisema baada ya kuwaondoa makocha hao, kikosi cha Pamba sasa kitakuwa chini ya Wilbert Mweta.

Desemba 23, mwaka huu Pamba ilifungwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam dhidi ya wenyeji Transit Camp.

Katika msimamo wa ligi hiyo inayochezwa kwa mtindo wa nyumbani na ugenini iko katika nafasi saba ikiwa na pointi 16 baada ya kushinda mechi nne, sare nne na kupoteza michezo minne wakati vinara ni DTB yenye pointi 30.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### BALE, ISCO KUONDOKA
MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 32, na kiungo wa kati wa Hispania, Isco (29), wataondoka Real Madrid Januari, huku mikataba ya wachezaji wote wawili ikimalizika msimu wa joto. ***(Marca)***

### MBAPPE AITEGA MADRID
REAL Madrid inazidi kuwa na uhakika wa kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe kutoka Paris St-Germain, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anaweza kusaini mkataba wa awali na klabu ya kigeni kuanzia Januari 1. ***(AS, via Mail)***

### RUDIGER MAMBO SAFI
REAL Madrid pia wanatarajia mlinzi wa Chelsea na Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28 atajiunga nao bila malipo mwishoni mwa msimu huu. Huku ikiwa imesalia miezi sita pekee katika mkataba wake. ***(Telegraph)***

### WANNE KUTUA UNITED
MANCHESTER United inalenga wachezaji wanne wa Ujerumani inaotarajia kuwasajili. Kiungo wa kati wa Bayer Leverkusen, Florian Wirtz mwenye miaka 18, mlinzi wa kushoto wa Borussia Monchengladbach (18), Luca Netz, kiungo wa kati wa RB Lepizig, Eric Martel na beki wa kati wa VFL Bochum Armel Bella-Kotchap (20), wote ni miongoni mwa wanaolengwa na kocha wa muda, Ralf Rangnick. ***(Sun)***

### KAMARA ANUKIA NEWCASTLE
NEWCASTLE United wanapanga kumsajili kiungo wa Marseille, Boubacar Kamara. Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 22 ni mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu, huku Manchester United na Chelsea pia zikivutiwa naye. ***(Sun)***

### MAITLAND KUTUA ROMA
KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kuondoka Arsenal na kujiunga na AS Roma ya Italia kwa mkopo. ***(Goal)***

### MOYES AMTAKA KELLY
KOCHA wa West Ham, David Moyes ana nia ya kumsajili beki wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 23 kutoka Bournemouth. ***(Telegraph)***

### GALLAGHER KURUDI CHELSEA
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amependekeza kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 21, atarejea Stamford Bridge kupigania nafasi yake baada ya kumalizika kwa mkopo wa muda mrefu katika klabu ya Crystal Palace. ***(Metro)***

### TERRY KUREJEA NYUMBANI
NAHODHA wa zamani wa Chelsea na England, John Terry anatarajiwa kurejea klabuni hapo kusaidia maendeleo ya vijana. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 41 aliacha nafasi yake kama msaidizi wa kocha wa wakati huo kule Aston Villa Dean Smith msimu wa joto. ***(Athletic)***

### ODOI ATAKIWA NAPOLI
WINGA wa Chelsea na England, Callum Hudson-Odoi mwenye umri wa miaka 21, analengwa na Napoli, ambayo inanolewa na kocha wa zamani wa Blues hao, Maurizio Sarri. ***(Tuttosport, via Football Italia)***

### BELLOTTI NJIA MOJA
MSHAMBULIAJI wa Italia, Andrea Belotti yuko tayari kuondoka Torino wakati mkataba wake na timu hiyo ya Serie A utakapokamilika msimu wa joto, huku AC Milan, Napoli na Fiorentina zikimwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Calciomercato, via Football Italia)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HATIMAYE COUTINHO AJIPELEKA ARSENAL

●●●Ni baada ya kuwapo kwa tetesi za kutakiwa na klabu...

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Barcelona, Philippe Coutinho anaripotiwa amewaambia Arsenal anataka kuungana nao kwenye dirisha la uhamisho la kipindi cha majira ya baridi, Januari.

Nyota huyu mwenye miaka 29 anatajwa kama mchezaji wa akiba kwa Barcelona wakati klabu hiyo ikiendelea kuweka sawa vitabu vyake vya fedha hapo Camp Nou.

Klabu kadhaa kutoka Ligi Kuu England zimeonyesha nia ya kuitaka huduma ya Coutinho wakiwamo Everton, Tottenham Hotspurs na Newcastle United.

Ripoti zimetaja wakala wa Countinho amekuwa na safari hivi karibuni kuzungumza na Arsenal juu ya uwezekano wa kuhamia klabuni hapo.

Kwa mujibu wa Sport nyota huyu ameichagua Arsenal kama klabu yake ijayo, hivyo Countinho anaweza kutua dimbani Emirates ambao wanaweza kufikia mahitaji ya mshahara wake.

Staa huyu wa zamani wa Liverpool ameweza kucheka na nyavu mara mbili pekee katika mechi 16 alizocheza, na amecheza kwa dakika tisa pekee kwenye mechi tatu za mwisho za La Liga.

MECHI KALI
HOME
AWAY
YOUNG AFRICANS
1.31 | 4.54 | 8.49
DODOMA FC
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE KASINO

# SANAMU YA RONALDO YAPIGWA ZENGWE

**GOA, India**

SANAMU mpya ya nyota wa soka wa Ureno, Cristiano Ronaldo, imepokelewa kwa hisia tofauti nchini India.

Sanamu hiyo imewekwa katika jimbo la Goa Magharibi, ambako mchezo wa soka ni maarufu sana, na maofisa wanatumaini itawatia moyo vijana.

Lakini Goa pia ni koloni la zamani la Ureno, na ni miaka 60 tangu jimbo hilo lilipokombolewa kutoka kwa taifa hilo.

Wakosoaji wanasema wachezaji nyota wa soka wa nchi hiyo wanastahili kutambuliwa, hasa ikizingatiwa wachezaji kadhaa wa zamani na wa sasa wa timu ya taifa ya India ni Wagoa.

"Nimesikitika sana kusikia sanamu ya Ronaldo imezinduliwa nchini. Tujifunze kujivunia sanamu za nyota wetu kama Samir Naik na Bruno Coutinho," kiongozi wa Wakazi wa Goa aliliambia Shirika la Habari la IANS.

Wakati wa uzinduzi wa sanamu hiyo, baadhi ya watu walipeperusha bendera nyeusi wakipinga, gazeti la Times nchini India liliripoti.

Timu ya soka ya Ureno ni maarufu sana katika jimbo la Goa, na kwa sababu ya ukoloni wake wa zamani, wenyeji wengi wameishi Ureno au wana familia huko.

Lakini baadhi ya watu katika jimbo hilo la India wanahisi ni makosa kuweka sanamu hiyo wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 60 ya Goa kupata uhuru wake kutoka kwa Ureno, ambayo ilifanyika miaka 14 baada ya sehemu zingine za India zilizobaki kukombolewa kutoka kwa utawala wa Waingereza.

"Kuweka sanamu ya mwanasoka wa Ureno mwaka huu ni kufuru. Tunalaani hili," IANS ilimnukuu mwanaharakati wa mrengo wa kulia, Guru Shirodkar alisema.

Michael Lobo, mbunge wa eneo hilo katika chama tawala cha Bharatiya Janata Party (BJP), aliweka picha yake kwenye ukurasa wa Twitter akiwa na sanamu hiyo, akisema ilikuwa imewekwa "kwa ombi la vijana wetu" ili kuwatia moyo "kupandisha viwango vya soka".

Ingawa kriketi inasalia kuwa mchezo maarufu zaidi wa India, kandanda - haswa Ligi Kuu England inapendwa katika maeneo kadhaa ya nchi - Kerala Kusini, Goa Magharibi, Bengal Magharibi Mashariki na majimbo yote manane ya Kaskazini-Mashariki.

Ronaldo, ambaye kwa sasa anachezea Manchester United, anapendwa na mashabiki wengi na anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora katika historia ya mchezo huo.

Hii sio mara ya kwanza kwa sanamu yake kuibua hisia, mnamo 2017 sanamu ya ajabu ya Ronaldo ilidhihakiwa na hatimaye kubadilishwa katika Uwanja wa Ndege wa Madeira nchini Ureno.



# Chilwell aipa pigo Chelsea


**LONDON, England**

CHELSEA imeweka wazi kuhusu beki wa klabu hiyo, Ben Chilwell kufanyiwa upasuaji wa goti na hivyo atakosa msimu uliobaki wa mwaka 2021/22.

Baada ya kupata jeraha la goti katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa dhidi ya Juventus, timu ya madaktari waliamua kumfanyia matibabu ya dawa yasiyo husisha upasuaji.

Lakini kutokana na kushindwa kupona timu ya madaktari ilifanya uamuzi wa pamoja wa wiki hii na kushauri Chilwell kufanyiwa upasuaji wa goti ili kutibu majeraha yake.

Chilwell alifanikiwa kucheza jumla ya michezo 12 ukijumuisha ule wa Ligi ya Mabingwa alioumia dhidi ya Juventus mnamo Novemba 23 na kufanikiwa kufunga mabao manne.



LIVE IN PLAY

# SPORTPESA WAIONGEZA MKATABA NAMUNGO FC

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo na burudani ya SportPesa Tanzania, imeongeza mkataba wa mwaka mmoja wa udhamini kwa Namungo FC ya Ruangwa, Lindi ambayo inashiriki Ligi Kuu Bara.

SportPesa imeingia makubaliano hayo ya kuendelea na kuidhamini Namungo baada ya pande mbili zote kufikia muafaka mzuri wa kuongeza mkataba.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa SportPesa, Tarimba Abbas, alisema wanafuraha kubwa kufikia makubaliano mazuri ya kuendelea kuidhamini Namungo.

Tarimba alisema mkataba wa mwaka mmoja wameingia na Namungo baada ya ule wa awali ukitarajiwa kumalizika mapema Januari, 2022.

"Tunaamini kwa kupitia udhamini huu tuliotoa Namungo utasaidia katika masuala ya maendeleo katika timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, kama SportPesa tutaendelea kuunga mkono mchezo wa soka kwa kupitia udhamini ambao tunaoutoa kutoka katika klabu mbalimbali zikiwamo klabu kubwa za Simba na Yanga," alisema Tarimba. Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Namungo, Omary Kaya, alisema "Tunaishukuru SportPesa kwa udhamini ambao imekuwa ikitupatia tangu ilipoanza kutudhamini".

"Hivyo tutaendelea kufanyakazi pamoja na SportPesa kwa kutimiza masharti ya kimkataba ikiwamo kuwatangaza vizuri".




Mkurugenzi wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas (kulia), akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Namungo, Omary Kaya, wameshika nakala za mkataba baada ya kampuni hiyo ya kubashiri kuongeza udhamini kwa klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Bara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba yatamba kuishusha Yanga

**Na Saada Akida**

HUKU timu yao ikiwa ndio wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano ya kimataifa, nahodha wa Simba, John Bocco, amesema kikosi chao hakina 'presha' na wao kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara ni suala la kusubiri muda 'utazungumza'.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Bocco alisema ushindani umeongezeka zaidi katika msimu huu na kupelekea mechi zote kuwa ngumu.

Bocco alisema malengo makubwa ya Simba ni kuhakikisha wanafanya vizuri katika kila mechi wanayocheza ili kupata pointi tatu zitakazowaweka katika mazingira mazuri.

"Kuelekea mchezo wetu dhidi ya Azam FC, tunajua utakuwa mgumu kwa sababu ya ubora wa wapinzani wetu, tunawaheshimu Azam lakini tutafuata maelekezo tuliopewa na mwalimu, naamini tutafanikiwa kufikia malengo yetu," alisema Bocco.

Kuhusu michuano ya kimataifa, Bocco alisema kila mchezaji wa Simba yuko tayari kucheza kwa bidii na hatimaye kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Simba, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara imepangwa katika Kundi D pamoja na timu za RS Berkane ya Morocco, Asec Mimosas kutoka Ivory Coast na US Gendarmerie ya Niger.

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA

PAKUA SASA

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 31 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2977 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Bnot Netanya W | 1.19 | 6.57 | 9.46 |
| 15:10 | 4341 | AL Baten vs Al Ittihad Jeddah | 3.28 | 3.53 | 2.08 |
| 15:30 | 2422 | AL Hazm vs AL Tai | 2.17 | 3.46 | 3.11 |
| 15:50 | 1082 | Al-Thaid vs AL Jazira AL Hamra | 2.13 | 3.60 | 2.83 |
| 15:50 | 1841 | Masfoot Sports Club vs Gulf FC | 1.97 | 3.67 | 3.13 |
| 15:50 | 1869 | Ahli Al-Fujirah vs City Football Club | 1.19 | 6.13 | 10.54 |
| 16:00 | 1071 | Emirates Club vs Al Sharjah SC | 6.15 | 5.00 | 1.36 |
| 16:00 | 1648 | Sectzya Nes Ziona vs Ahi Nazareth | 1.91 | 3.52 | 3.81 |
| 16:00 | 3107 | Zanaco vs Red Arrows | 2.41 | 2.80 | 3.04 |
| 16:00 | 4214 | Hapoel Afula vs Hapoel Acre | 3.22 | 3.17 | 2.25 |
| 16:00 | 4311 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Ittihad Kalba | 2.25 | 3.42 | 2.75 |
| 16:00 | 4543 | Markez Balata vs Islami Qalqilya | 2.15 | 3.40 | 3.35 |
| 16:00 | 4931 | SC Kfar Qasem vs El Fahem | 2.36 | 2.91 | 3.31 |
| 16:00 | 5283 | Bnei Yehuda vs Beitar Tel Aviv Ramla | 1.60 | 3.76 | 5.54 |
| 16:00 | 5386 | Hapoel Raanana vs Ironi Hasharon | 2.34 | 3.01 | 3.21 |
| 16:00 | 5904 | Real Oviedo vs Ponferradina | 2.28 | 2.95 | 3.30 |
| 16:10 | 1602 | Al Kuwait SC vs AL Nasr | 1.49 | 4.03 | 5.57 |
| 17:00 | 1465 | RC Kouba vs SC Ain Defla | 1.19 | 5.60 | 12.55 |
| 17:00 | 1693 | JSM Tiaret vs ASM Oran | 1.96 | 3.08 | 3.75 |
| 17:00 | 2315 | JSM Bejaia vs JS Bordj Menaiel | 1.92 | 3.13 | 3.85 |
| 17:00 | 2327 | MC Saida vs USM Hadjout | 1.55 | 3.56 | 5.77 |
| 17:00 | 2804 | MCB Oued Sly vs USM Bel Abbes | 1.38 | 4.25 | 7.14 |
| 17:00 | 2993 | CA Bordj Bou Arreridj vs CA Batna | 2.44 | 2.97 | 2.83 |
| 17:00 | 3118 | MC EL Eulma vs MO Constantine | 1.89 | 3.09 | 4.05 |
| 17:00 | 3127 | CRB Ain Ouessara vs USM EL Harrach | 2.11 | 2.93 | 3.51 |
| 17:00 | 3686 | Ben Aknoun vs GC Mascara | 1.77 | 3.13 | 4.62 |
| 17:00 | 3833 | Skaf Khemis Miliana vs WA Boufarik | 2.39 | 2.85 | 3.45 |
| 17:00 | 3955 | Knockbreda vs H and W Welders | 2.70 | 3.77 | 2.15 |
| 17:00 | 3993 | Hamra Annaba vs MO Bejaia | 2.01 | 2.90 | 3.87 |
| 17:00 | 4196 | USM Khenchela vs USM Annaba | 2.01 | 2.90 | 3.87 |
| 17:00 | 4329 | ZR Temouchent vs El Bayadh | 1.73 | 3.28 | 4.63 |
| 17:00 | 5012 | IRB Lakhdaria vs US Chaouia | 2.45 | 2.84 | 2.94 |
| 17:00 | 5306 | Ain M'lila vs NRB Teleghma | 2.32 | 2.94 | 3.04 |
| 17:00 | 5924 | Irb Ouargla vs JSM Skikda | 1.66 | 3.43 | 4.83 |
| 17:35 | 1704 | Al-Ettifaq vs AL Faiha | 1.94 | 3.51 | 3.71 |
| 18:00 | 4031 | Hilal Al-Quds vs Mosaset AL Bireh | 1.64 | 3.46 | 5.00 |
| 18:00 | 4713 | Burgos vs Amorebieta | 2.26 | 3.09 | 3.18 |
| 18:05 | 3920 | Al Faisaly (KSA) vs Al Hilal Riyadh | 4.16 | 3.76 | 1.77 |
| 18:15 | 2191 | Valencia vs Espanyol | 1.77 | 3.65 | 4.51 |
| 18:15 | 5972 | Eibar vs Real Sociedad B | 1.63 | 3.70 | 5.13 |
| 18:30 | 4957 | AL Wahda Scc (UAE) vs Jazira Abu Dhabi | 2.22 | 3.51 | 2.74 |
| 18:35 | 4509 | Salah vs Fanja Club | 3.77 | 3.38 | 1.86 |
| 18:45 | 5833 | Al Salmiyah vs Yarmouk | 1.43 | 4.51 | 5.57 |
| 19:00 | 5853 | Young Africans vs Dodoma FC | 1.31 | 4.54 | 8.49 |
| 20:00 | 2555 | Rio Ave vs Covilha | 2.04 | 3.18 | 3.57 |

JUMAMOSI - 01 - JANUARI 2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 09:05 | 1117 | WS Wanderers FC W vs Canberra United W | 2.89 | 3.66 | 2.08 |
| 11:45 | 4289 | Adelaide United vs Wellington Phoenix | 1.98 | 3.64 | 3.39 |
| 13:00 | 2958 | Shahrdari Astara vs Vista Turbine | 1.96 | 2.61 | 4.83 |
| 13:30 | 1077 | Shams Azar Qazvin vs Esteghlal Mollasani | 1.84 | 2.80 | 5.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Desemba 31, 2021
Nipashe



UKURASA 21

## Hatimaye Coutinho ajipeleka Arsenal




Kiungo mshambuliaji mpya wa Azam FC, Ibrahim Ajib akionyesha jezi yake atakayoitumia baada ya kusaini mkataba wa mwaka mmoja wa kuitumikia timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara. **PICHA: MTANDAO**

## Pablo 'kushusha' majembe manne

**Na SaadaAkida**

WAKATI joto la mechi dhidi ya Azam FC likizidi kupanda, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema amekiandaa vyema kikosi chake lakini anahitaji kuongeza nyota watano wapya ili kuimarisha timu yake inayotetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Pablo alisema hayo jana lakini aliongeza kikosi chake kiko tayari kuwavaa Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kocha huyo alisema baada ya kuwapa wachezaji wake mapumziko ya siku mbili, walirejea tena mazoezini juzi kuendelea kujiimarisha ili kuwakabili Azam FC.

Alisema kila mchezaji yuko tayari kwa ajili ya mchezo huo na wanatambua utakuwa mgumu na wenye ushindani kwa sababu kila upande unahitaji kupata matokeo chanya na hatimaye kukaribia malengo ya kuwania ubingwa.

"Utakuwa mchezo mgumu na wenye ushindani mkubwa, tuko tayari kwa ajili ya mchezo huo, tunachohitaji ni pointi tatu muhimu," alisema Pablo.

Kuhusu wachezaji ambao hawatakuwepo ni wale majeruhi huku akiweka wazi maendeleo ya Taddeo Lwanga kwamba yanaendelea vizuri ingawa bado yuko chini ya uangalizi wa madaktari.

"Mbali na wagonjwa kuna nyota wengine (hakutaja majina yao) wameruhusiwa kwenda kutafuta changamoto nyingine na suala la usajili tutaongeza kati ya wanne au watano, nafasi moja ikiwa ni kiungo na beki," alisema kocha huyo.

Tayari nyota wanne wa Simba wanatajwa wameachana na kikosi hicho ambao ni pamoja na Abdulswamadu Kassim, Jeremia Kisubi, Duncan Nyoni na Ibrahim Ajib ambaye jana alitambulishwa kujiunga na Azam FC.

# YANGA, DODOMA JIJI HAPATOSHI

### ●●●Makocha watambiana katika mechi hiyo ya kufunga mwaka ambayo...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

KUELEKEA mechi ya kufunga mwaka 2021 ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, kocha wa Yanga, Cedric Kaze na Renatus Shija wa Dodoma Jiji FC, kila mmoja ametamba timu yake itapambana kuhakikisha inaondoka na pointi tatu huku pia wakiahidi soka la burudani katika mchezo huo.

Yanga ndio mwenyeji wa mchezo huo utakaochezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Vinara wa ligi hiyo, Yanga watashuka dimbani bila ya wachezaji wake wawili, Djuma Shaban na Djigui Diarra ambao wameenda kujiunga na timu zao za Taifa (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo-DRC na Mali).

Akizungumza jijini jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Kaze alisema wamejiandaa vizuri kuwakabili Dodoma Jiji FC timu ambayo wanacheza soka la ushindani kila wanapokutana.

"Dodoma Jiji FC ni timu ngumu na ina uzoefu katika ligi lakini pia timu inayojilinda sana, tunatakiwa kuonyesha kiwango kizuri ili kupata matokeo chanya dhidi ya wapinzani hawa," alisema Kaze.

Kocha huyo alisema tayari wameshapata wachezaji watakaoziba nafasi ya Djuma na Diarra na hawana wasiwasi na mabadiliko hayo.

"Kuhusu kipa mpya, Aboutwalib Mshery, kucheza ni asilimia ndogo kwa sababu kuna taratibu za utendaji bado hazijakaa sawa na nafasi ya Diarra atacheza Eric Johora," alisema Kaze.

Naye Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji FC, Shija, alisema wamejiandaa kufanya vizuri katika mechi hiyo baada ya kuangalia ubora na udhaifu wa Yanga huku pia wakijipanga kucheza kwa tahadhari.

Shija alisema ubora wa Yanga uko sehemu tatu ikiwamo safu ya kiungo, pembeni na upigaji wa krosi jambo ambalo wamefanyia kazi kwa siku tatu baada ya kuwahi kuwasili jijini.

"Tumewaandaa vijana wetu katika kila idara ikiwamo sehemu hizo tatu, msimu huu Dodoma Jiji FC tunacheza mpira mwingine tofauti na msimu uliopita, tutawaonyesha Yanga soka la Ujerumani, tumejiandaa kwa mbinu na ufundi, tunaenda kuharibu furaha ya Yanga, kuwasimamisha na kumaliza mwaka kwa majonzi ," alisema Shija.

Aliongeza kuhusu uamuzi wa kuwatumia wachezaji wapya waliosajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo akiwamo, Waziri Junior, alieleza hilo litatokana na aina ya uchezaji ambao wapinzani wao Yanga wataingia nao.

Nahodha wa Dodoma Jiji FC, Mbwana Kibacha, alisema "Morali ya wachezaji iko vizuri na mwalimu amemaliza majukumu yake, kazi kubwa imebaki kwetu kwenda kufanya kile tulichoelekezwa mazoezini,".

Wakati huo huo, baada ya kutangaza kusajili wachezaji wawili wapya, Salum Aboubakar 'Sureboy' kutoka Azam FC na Aboutwalib Mshery akitokea Mtibwa Sugar, Yanga imesema itatangaza nyota wake wengine wawili kabla ya kufungwa usajili wao katika kipindi hiki cha dirisha dogo. Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema wachezaji wote wamesajiliwa kwa mapendekezo ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi huku akiweka wazi tayari kipa wao mpya, Mshery, ameshaingia kambini na kuanza mazoezi ya wenzake.

Nyota mwingine ambaye anakaribia kutua Yanga ni winga wa Biashara United, Dennis Nkane, ambaye katika mechi iliyopita wakati timu hizo zilipokutana, alikuwa jukwaani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >